# Nipashe

Jumatano Agosti 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581040

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,023,154,178/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mshtakiwa** kesi ya Zumaridi akiri kutenda makosa

UKURASA 3



ALLEGRI HANA WASIWASI NA JERAHA LA DI MARIA

UKURASA 22

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



# Miili ya watu yaokotwa ikiwa kwenye viroba

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

**HUDUMA BOLT SASA KWA WENYE KADI PEKEE**

KAMPUNI ya usafirishaji abiria ya Bolt, imesema kuanzia leo itaanza kutoa huduma...

## 'Sarakasi' zaendelea NCCR Mageuzi

UKURASA 3



Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi, Martha Chiomba (katikati), akiongoza kikao cha baadhi ya wajumbe wa chama hicho wanaomuunga mkono katika ofisi za makao makuu yao Ilala jijini Dar es Salaam jana. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa chama hicho, Joseph Selasini. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

Baadhi ya wakazi wa Inyala wilayani Mbeya, wakichungulia ndani ya basi la Kampuni ya Super Rojas, ambalo ni miongoni mwa magari yaliyotumbukia mtoni, baada ya kugongwa na lori lililofeli breki na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 10, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**



# Lori laparamia magari matatu na kuua zaidi ya watu 10

UKURASA 2

**MICHEZO** DEJAN ATOA AHADI YA MABAO SIMBA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Miili ya watu yaokotwa ikiwa kwenye viroba

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MIILI ya watu watatu imeokotwa ikiwa imefungiwa kwenye mifuko ya sandarusi maarufu viroba, baada ya kutupwa na watu wasiojulikana katika Kitongoji cha Dibabara, Kijiji cha Kwastemba, Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga.

Inaelezwa kuwa, mwili mmoja uliokotwa katika Kata ya Tunguli, baada ya gari moja aina ya Toyota Landcruiser kupita katika eneo la Dibabara, Agosti 11 mwaka huu majira ya saa moja usiku.

Alipotafutwa kuzungumzia taarifa za kuokotwa kwa miili hiyo, Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Safia Jongo, alisema anafuatilia matukio hayo na atatoa taarifa kwa vyombo vya habari wakati wowote.

Katika tukio la kwanza, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Tunguli, Omary Mtoi, alidai kuwa wakazi wa Kitongoji cha Dibabara, ambao ni jamii ya wafugaji ya Kimasai, waliona gari lenye rangi nyeupe aina ya Toyota Landcruser, likiingia maeneo ya kitongoji hicho, lakini hawakujua kuna nini na linaenda wapi.

"Kwa muda huo hakuna mtu aliyeshughulika na gari hilo, kila mmoja aliona ni kawaida. Kwa hiyo hawakuchukua namba zake za usajili, ila waliona gari jeupe likipita," alieleza Mtoi.

Alisema asubuhi yake, walishtuka baada ya kuona viroba vimetelekezwa kilomita chache kutoka barabara kuu iendayo Songe, makao makuu ya Wilaya ya Kilindi na Gairo.

"Nilipovisogelea hivyo viroba na kuvifungua, niliona miili ya watu. Baada ya hapo, nilitoa taarifa ofisi ya kata, ambayo nayo iliripoti tukio hilo Kituo cha Polisi Kikunde. Walifika na kushuhudia unyama huo na kwa kuwa hawakufahamika kwenye eneo hilo na la jirani hivyo waliamua kuipeleka miili hiyo katika machimbo ya Seita kwa utambuzi.

"Wale watu walionekana kama wachimbaji na ndiyo maana wakapelekwa mgodini lakini cha ajabu hakuna aliyetambuliwa na ndipo polisi wakaamua kwenda kuihifadhi katika hospitali ya wilaya," alisema.

Inaporejewa historia ya matukio ya aina hiyo, mwaka 2017, kuliripotiwa nchini matukio kadhaa ya kuonekana maiti za bindamu zikiwa zimefungwa kwenye mifuko ya sandarusi.

Hata hivyo, kipindi hicho miili hiyo ilikuwa inaopolewa ikiwa kwenye mifuko hiyo katika Mto Ruvu mkoani Pwani na baadhi ya fukwe za Bahari ya Hindi mkoani Dar es Salaam.

Katika ufafanuzi wake kuhusu suala hilo, Jeshi la Polisi lilisema lilikuwa linafanya uchunguzi huku likiwaomba watu waliokuwa wamepotelewa na ndugu zao, kujitokeza kupima vinasaba katika jitihada za utambuzi wa miili iliyokuwa inaopolewa.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) katika tamko lake la Agosti 25, 2017, pia kiligusia suala la kuonekana kwa maiti za binadamu zikiwa ndani ya mifuko hiyo ikielea katika mito na Bahari ya Hindi bila kujulikana ni watu gani na ni nani anayewaua.

Chini ya Mkurugenzi Mtendaji wake, Anna Henga, kituo hicho kiliitaka Ofisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai kufanya uchunguzi wa miili na matukio hayo ili kutoa taarifa sahihi ambayo ingewatoa hofu wananchi kwa kuwa vitendo vya mauaji ya kinyama dhidi ya binadamu kama hayo ni uvunjifu mkubwa wa sheria na haki za binadamu na Watanzania wana haki ya kufahamu matukio hayo yanafanywa na watu gani.



Daktari wa Macho, Andrew Kilumbi (kulia), akifanya upasuaji wa jicho la mgonjwa katika kambi maalum iliyoratibiwa na Dar es Salaam Mzizima Lions Club kwenye Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Odinga avunja ukimya, apinga matokeo urais

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais kupitia Muungano wa Azimio Kenya, Raila Odinga, amepinga matokeo ya uchaguzi yaliyomtangaza Naibu wa Rais, William Ruto, kuwa ndiye Rais mteule wa nchi hiyo na kutangaza kuchukua hatua za kisheria.

Juzi, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati, alimtangaza mgombea urais kupitia Kenya Kwanza, Dk. William Ruto, kuwa mshindi kwa kupata kura milioni 7.1 (asilimia 50.49) dhidi ya kura milioni 6.9 (asilimia 48.85) alizopata Odinga.

Wagombea wengine kwenye uchaguzi huo walikuwa ni Prof. George Wajackoyah aliyepata kura 61,969 (asilimia 0.44) na David Waihiga kura 31,987 (asilimia 0.23).

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Nairobi, Odinga aliyekuwa anawania urais kwa mara ya tano akianzia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1997 na kote akiangushwa na wapinzani wake, alisema atakwenda mahakamani kupinga matokeo hayo.

Alisema hawatakubali kuona mtu mmoja anajaribu kuleta vurugu katika taifa na kutaka kubadilisha yale ambayo Wakenya waliamua.

"Ninataka kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa Wakenya wenzangu ambao wameshiriki katika uchaguzi uliopita walionyesha ujasiri, uzalendo na upendo kwa nchi yao, Wakenya kila mahali walijitokeza wakapiga kura kwa njia ya amani," alisema.

Odinga alisema wamegundua hitilafu ambayo ilifanyika katika tume ambayo ilijaribu kukiuka yale ambayo Wakenya walikuwa wamefanya.

Pia alisema wameona yaliyofanywa na Mwenyekiti wa IEBC kwa kujaribu kupindua uamuzi wa Wakenya.

Awali, Makamishna wanne wa IEBC wakiongozwa na Naibu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Juliana Cherera, walipinga kuyatambua matokeo yaliyotangazwa, wakiwaeleza waandishi wa habari kuwa jumla ya kura zilizotangazwa inafika asilimia 100.01 na kwamba hayaakisi maoni ya makamishna ambayo yalipaswa kushughulikiwa na kukubaliana kabla ya kutangazwa.

Makamishna wengine ni Francis Wanderi, Irene Masit na Justus Nyang'aya na katika tamko lao la pamoja walisema: "Hii inatupa jumla ya asilimia 100.01, ina maana takribani kura 142,000 ambazo zitafanya tofauti kubwa katika matokeo ya mwisho, tulipotaka tuhakiki matokeo, mwenyekiti alikataa na kusisitiza kutangaza matokeo."

Rais Samia Suluhu Hassan amewapongeza wananchi wa Kenya kwa kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu ambao matokeo yake, Dk. William Ruto ametangazwa kuwa Rais mteule.

***Imeandikwa na Romana Mallya na Maulid Mmbaga**

# Lori lilivyoparamia magari, kuua zaidi ya watu 10

**Nebart Msokwa na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya watu 10 wamefariki dunia huku wengine ambao idadi yao haijafahamika wakijeruhiwa mkoani hapo baada ya lori la mizigo lililokuwa limesheheni mchanga wa dhahabu, kufeli breki katika eneo la Inyala nje kidogo ya Jiji la Mbeya na kuparamia magari matatu.

Kati ya magari yaliyogongwa na lori hilo ni basi la abiria mali ya Kampuni ya Super Rojas linalofanya safari zake kati ya Mbeya na Njombe, lori lingine la mizigo pamoja na gari moja ndogo.

Ajali hiyo ilitokea jana asubuhi katika eneo la Shamwengo na baada ya lori hilo kuyagonga magari hayo lilitumbukia korongoni huku mengine yaliyogongwa yakitolewa nje ya barabara.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema chanzo cha ajali hiyo ni lori hilo lenye namba za usajili T. 387 DFJ kufeli breki kwenye mteremko huo.

Alisema wengi wa waliofariki kwenye ajali hiyo walikuwa kwenye basi la Kampuni ya Super Rojas na majeruhi walipelekwa hospitali za Igawilo na Inyala, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

"Majeruhi tumewapakia kwenye lori kwa ajili ya kuwakimbiza hospitalini, kwa sasa hatujapata idadi kamili ya vifo na majeruhi kwa sababu kazi kubwa iliyokuwa inafanyika ni kuokoa maisha ya watu, tukitoka hapa tutafuatilia na tutatoa taarifa," alisema Kamanda Matei.

Alisema lori hilo lingeleta madhara zaidi endapo lingeendelea kushuka chini kwa maelezo kuwa lilipunguza madhara baada ya kugonga lori lingine lililokuwa linapandisha juu kuhama njia na kutumbukia kwenye korongo.

Alisema tatizo lililoko kwenye eneo hilo lina mteremko mkali na barabara ni nyembamba hali ambayo inafanya malori yanayofeli breki yashindwe kupita bila kusababisha madhara.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Igawilo, Dk. Grace Dugo, alikiri kupokea maiti tisa na majeruhi wawili ambao mmoja alifariki wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

"Hadi sasa tumepokea maiti 10 kati yao wanawake watatu na wanaume saba na kwamba tunaandaa utaratibu wa kumpeleka kwenye matibabu zaidi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya kwa ajili ya matibabu zaidi baada ya kuvunjika miguu," alisema Dk. Dugo.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo walisema baada ya lori hilo kufeli breki lilikuwa linashuka kwenye mteremko huo kwa kasi isiyokuwa ya kawaida.

Mmoja wa mashuhuda hao, Marekani Mwahalemba alisema alishuhudia lori hilo likiteremka kwa kasi huku likiyagonga magari mengine.

Alisema yeye alikuwa kwenye usafiri wa bajaji akitokea Shimwengo kuelekea Inyala, lakini baada ya kuona lori hilo likishuka kwa kasi walilazimika kupaki pembeni.

Pia, alisema alishuhudia gari la abiria kampuni ya Super Rojas, likitumbukia mtoni na kusababisha vifo na majeruhi.

Joseph Samwel, aliiomba serikali kuharakisha upanuzi wa barabara katika eneo hilo ili kuepusha ajali za mara kwa mara ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu.

HABARI KITAIFA

# ‘Sarakasi’ za NCCR-Mageuzi zashika kasi

**Na Elizabeth Zaya**

SARAKASI ndani ya Chama cha NCCR-Mageuzi zimezidi kushika kasi kwa kila upande kutamba wako kihalali na wana mamlaka ya kuendeleza shughuli za chama, licha ya kuonekana mgawanyiko na kutoelewana baina yao.

Hivi karibuni, baada ya Halmashauri Kuu inayomuunga mkono Mwenyekiti wa Chama hicho, James Mbatia, ilisema haiwatambui Katibu Mkuu Martha Chiomba na wanaomuunga mkono.

Aidha, waliwataka warudishe ofisi kwa viongozi halali (Mbatia na wenzake) lakini jana katibu mkuu huyo alieleza msimamo wa kundi lake kuwa wao ni viongozi halali na hawataondoka kwenye ofisi hizo.

Maazimio mengine ambayo yalifikiwa na halmashauri kuu inayomuunga mkono Mbatia katika kikao kilichofanyika Agosti 14, mwaka huu, ni pamoja na kutengua uamuzi wa kumvua Mbatia na Makamu Mwenyekiti wake Bara, Angelina Mtahiwa, ambao walisimamishwa na Halmashauri Kuu inayomuunga mkono Chiomba.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkuu wa Idara ya Uenezi na Uhusiano wa Umma wa chama hicho anayemuunga mkono Mbatia, Edward Simbeye, alisema baada ya uamuzi huo wa halmashauri kuu, kinachofuata ni kuwaita viongozi hao katika kamati maalum iliyoundwa ili kuwapa nafasi ya kujitetea kwa nini wasifukuzwe uanachama. Simbeye alisema kitendo cha Chiomba kupingana na uamuzi wa Halmashauri Kuu hakina tija kwa sababu ndiyo iliyomchagua na ina mamlaka ya kumtoa.

Kwa upande wake, Chiomba alisema: “Mimi bado ni katibu mkuu na hawezi kusikiliza wala kutekeleza maagizo ya watu ambao si viongozi halali wa chama.

“Sisi tunasema kile kilichofanyika juzi Agosti 13 na upande wa pili ni batili (unaomuunga mkono Mbatia), si kikao halali na hakina wajumbe halali. Mwenyekiti (Mbatia) amesimamishwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zetu.”

“Kikao cha tarehe 21 Mei cha Halmashauri Kuu ambacho kilimsimamisha Mbatia na wenzake kilikuwa halali na kila kitu kilipelekwa ofisi ya msajili wa vyama vya siasa na yenyewe ikathibitisha kupitia barua ya Mei 25, mwaka huu kwamba Mbatia na wenzake waliosimamishwa, wasijihusishe na shughuli za chama na wakifanya hivyo ni kinyume cha sheria” alisema.

Chiomba alisema hawajaitwa na kamati kuu yoyote kwenda kujitetea kama ilivyoelezwa na upande wa pili wa chama hicho unaomuunga mkono Mbatia.

Nipashe lilishuhudia katibu mkuu huyo akiongoza kikao na baadhi ya wajumbe ambao idadi yao ilikuwa 10 ndani ya ofisi ya chama hicho iliyopo wilayani Ilala, ambacho alisema ni kwa ajili ya maandalizi ya mkutano mkuu.

Mei 22 mwaka huu, Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi inayomuunga mkono Martha, iliwasimamisha uongozi Mbatia na Makamu wake Tanzania Bara, kutojihusisha na shughuli za chama kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo ukiukwaji wa maadili, kuwagombanisha viongozi wa chama hicho na kuwalazimisha wasaini kujiuzulu.

KESI YA ZUMARIDI

# Mshtakiwa akiri kutenda kosa

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

MSHTAKIWA wa 17, Hildegard Stanslaus, katika kesi ya jinai namba 12 ya mwaka 2022 inayomkabili Mchungaji Diana Bundala maarufu Mfalme Zumaridi, mkazi wa jijini Mwanza na wenzake 84, amekiri mahakamani kuwashambulia maofisa wa umma na kuwasababishia majeraha.

Hata hivyo, baada ya kukiri kutenda kosa hilo jana mahakamani, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, Crescensia Mushi, alilazimika kuahirisha kesi hiyo kwa saa moja baada ya kelele kutawala ukumbi wa mahakama.

Hayo yalitokea jana katika mahakama hiyo baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka na hakimu kumtaka akiri kama alifanya kosa hilo au akane kama hakufanya.

Mshtakiwa huyo alikiri kosa lake na kuiambia mahakama kwamba siku ya tukio akiwa na waumini wenzake, walishirikiana kuwaita na kuwachokoza askari na kisha kuanza kuwashambulia.

Baada ya mshtakiwa huyo kukiri kutenda kosa hilo, kulizuka sintofahamu baada ya mshtakiwa namba moja, Mfalme Zumaridi, kutamka maneno kwa sauti ya juu ndani ya mahakama, akimtaka mshtakiwa mwenzake kukana kutenda kosa.

Kutokana na kelele hizo, hakimu aliahirisha kesi hiyo kwa muda wa saa moja kumpa nafasi ili wakili wa utetezi nafasi ya kuongea na mteja wake kujiridhisha kuhusu ya afya ya akili ya mteja wake.

Baada ya mapumziko hayo ya saa moja, mahakama ilirejea na kuendelea na mahojiano na washtakiwa wengine, wote wakikana kosa huku mshtakiwa namba 17 akiachwa pasi na kuulizwa chochote.

Zumaridi na wenzake walikamatwa Februari 23, 2022 katika Mtaa wa Buguku, Kata ya Buhongwa jijini Mwanza na kufunguliwa mashtaka mbalimbali ya jinai, yakiwamo kufanya mkusanyiko bila kibali, kushambulia maofisa wa umma na kuzuia maofisa wa serikali kutekeleza majukumu yao.

Kesi hiyo inayosikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza mbele ya Hakimu Crescensia, iliitwa jana kwa ajili ya kuendelea na usikilizaji wa mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri unaongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Dorcas Akyoo, akisaidiana na Deogratius Rumanyika huku mawakili wa upande wa utetezi wakiongozwa na Steven Kitare.

**Imeandikwa na Vitus Audax na Pelusy Yohana (SAUT)**


## Forever Remembered, Forever Missed



216997001

**Basil Pesambili Mramba**
**Born: 15th May, 1940 Departed: 17th August, 2021**

Dear Lord, we lost our father a year ago. We still feel his presence in all we do even though it has been one year since you left us. The heartache feels like it will never heal, but through the countless moments he touched our lives and those around us. We find solace in the beautiful memories we will forever hold. Those cherished moments came with a lot of love and care.

He knows we will always love and care for him even as he rests with the angels. Lord, please take care of him as he was the only one we had.

We miss you, dad. Your work touched many. You blessed many, and we are blessed to call you our dad.

Fondly remembered by your wife and children Mrs. Awaichi Mramba, Godfrey, Dr. Aifena, Remla and Lilian; your in-laws Kerri, Evans, Vincent and George; your grandchildren Mattias, Elisia, Alexia, Aris, Andre, Malia, Mwami and Sia and many other close families and friends.

***Isaiah 41:10: “Do not fear, for I am with you; do not dismay, for I am your God. I will strengthen you and help you; I will uphold you with my righteous right hand.”***



NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA UMMA JUU YA OFISI MPYA YA MAKAO MAKUU YA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

1. Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linapenda kuutangazia Umma na Wafanyakazi wote wa NHC kuwa kuanzia tarehe 15 Agosti Ofisi ya Makao Makuu ya NHC na Ofisi za Mkoa wa Dodoma zilizopo Mtaa wa Medeli Magharibi, Jijini Dodoma sasa zimehamia katika Jengo la **MKANDARASI PLACE** ghorofa ya Sita.

2. Hivyo, kuanzia Agosti 15, 2022 shughuli zote za NHC Makao Makuu na Mkoa wa Dodoma zinafanyika katika Ofisi hiyo mpya ya Jengo la **MKANDARASI PLACE** iliyopo jirani na **TREASURY SQUARE.**

3. Kwa taarifa hii, mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

**MKURUGENZI MKUU**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**
**S.L.P 2422**
**MKANDARASI PLACE,**
**DODOMA**

**AU**

**MENEJA WA MKOA**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**
**S.L.P 391,**
**MKANDARASI PLACE**
**DODOMA**

**Baruapepe: dg@nhc.co.tz**
**Tovuti www.nhc.co.tz**
**Simu: +255262962361**

216996601

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

TANESCO

# MRADI WA KUFUA UMEME

- **Waziri, Mhandisi Mkazi wafunguka siri ya mageuzi makubwa ndani ya mwaka, wataja mambo mawili yanayowasimamia**

*Na Sanula Athanas*

KWA sasa mtu anapoutaja Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), moja kwa moja anagusa miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea kitaifa hivi sasa.

Bila kusahau, katika upande wa pili wa sarafu, kuna mikono inayonyooshwa na maswali nyuma yake dhidi yake; mahususi ikigusa kasi ya maendeleo yake na suala la mazingira, hususan kulikokuwa Pori Tengefu la Selous ambalo ni hazina ya taifa.

Wiki iliyopita, Nipashe ilikuwa sehemu ya ugeni maalum uliozuru eneo hilo lenye mradi huo mkubwa na wa kimkakati ndani ya Hifadhi mpya ya Taifa ya Nyerere.

Inaporejewa historia, mradi huo awali ulibatizwa jina la mwasisi wake, Stiegler's Gorge katika zama za uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Kwanini umma unahoji kasi na uhalali wa mradi huo? Hapo Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, anatoa majibu mafupi kwamba wana haki zote za kuhoji hayo.

"Mradi huu ni mkubwa na kiu ya Watanzania ni kuona unaanza uzalishaji wa umeme. Unapoona watu wanahoji maendeleo yake, hupati hofu kwa sababu ni haki yao na kikubwa tunausimamia kuhakikisha unakamilika na kuanza kuzalisha umeme."

Katika hilo, Waziri mwenye dhamana na Nishati, January Makamba, ambaye katika ziara yake aliambataha na Bodi nzima ya TANESCO, anatetea uhalali wa kimazingira kwamba ulinganifu uliopo kati ya kinachoathirika kimazingira katika eneo hilo dhidi ya ongezeko la umeme kitaifa litakalopatikana, una asilimia kubwa ya manufaa kwa sura pana ya kitaifa kutokana na ongezeko la umeme kulinganishwa na kidogo kinachonyooshewa kidole kimazingira.

"Mradi huo ukikamilika utasaidia kupatikana umeme mwingi wa gharama nafuu hivyo kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambayo ni hatari katika uhifadhi wa misitu na mazingira kwa ujumla. Hivyo, ni hatari zaidi kutokutekeleza mrad huu kuliko kuutekeleza," anafafanua.

Waziri January anaeleza kwamba mradi huo ambao mkataba wake ulitiwa saini wiki mbili kabla ya kuanza mwaka 2019 na ukaanza kutekelezwa rasmi miezi sita baadaye (Juni 14, 2019), sasa umeshika kasi kubwa kiutekelezaji.



*Waziri wa Nishati, January Makamba, akiwafafanulia jambo wajumbe wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na waandishi wa habari waliotembelea Bwawa la Julius Nyerere wiki iliyopita.*

Hapo ana maana kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, utekelezaji wa mradi umepiga hatua mara mbili ya ulivyokuwa umefikia kipindi cha kabla ya hicho, Juni 2021.

Anabainisha kuwa kwa sasa mradi umefikia asilimia 67.18, ilhali hadi Juni mwaka jana, ulikuwa umefikia asilimia 30 ya utekelezaji wake. Kiwango hicho kilichofikiwa ni sawa na theluthi mbili ya safari ya mradi kutimia.

**MAENEO MANANE YA MRADI**

Mhandisi Mkazi wa mradi huo, Lutengano Mwandambo, ana ufafanuzi wake uliozama zaidi katika stadi za uhandisi, anajikita katika orodha ya mambo manane.

Eneo la kwanza analolitaja ni kazi ya kuchepusha mto katika harakati za kutengeneza maporomoko ya maji ya kuzalisha umeme, iko katika hatua za mwisho za kukamilika, hadi sasa imefikia asilimia 97.35.

Mwandambo anataja eneo lingine ni kazi ya kujenga tuta kuu la maporomoko ya maji ambayo imefikia (asilimia 78.08).

Mhandisi Mkazi analitaja eneo la tatu ni kazi ya ujenzi wa jengo la mitambo, maarufu Powerhouse, ambalo kazi yake hadi sasa imefikia asilimia 51.11.

Pia, anafafanua kuwapo kwa ujenzi wa njia maalum za mtiririko wa maji ya kuendesha mitambo (Power Waterways) unaosababisha msukumo kwa kuendesha mitambo inayozalisha umeme. Kazi hiyo imefikia asilimia 85.46.

Sambamba na kazi hizo, Mwandambo anataja kazi ya tano inayoendelea ni ujenzi wa Kituo cha Kusafirisha Umeme (Switchyard) unaopokewa kutoka kwenye mitambo, ambayo sasa imefikia asilimia 89.7.

Kazi ya sita anayoitaja ni ujenzi wa kingo za bwawa (saddle dams) ambazo zinalinda mto na kuhifadhi maji yake, daima bwawa lisobomoke na kutengeneza mto mwingine unaochepusha maji. Hapo safari ya ujenzi nayo imefikia asilimia 54.12.

Kazi za saba na nane za mradi huo ni ujenzi wa miundombinu inayouhudumia mradi ndani ya mazingira yake na kuunganisha na maeneo mengine ya nchi.

Hapo Mhandishi Mkazi Mwanadambo anaitaja kuwa ni ujenzi wa barabara za kudumu kwenye mradi upande mmoja, ukiendana na ujenzi wa daraja lake la kudumu ambalo analipa sifa kwamba ni la pili kwa ukubwa kwenye Mto Rufiji, la kwanza linajulikana ni Daraja la Mkapa linalounganisha maeneo ya Ikwiriri na Muhoro.

Vivyo hivyo, Mhandisi Mkazi Mwandambo ambaye anasema kazi hiyo ya ujenzi wa miundombinu inakwenda sambamba na ujenzi wa makazi ya kudumu na ofisi. Hadi sasa mradi umeajiri watu 12,000.

**MATARAJIO YA MRADI**

Mradi huo unaokadiriwa kugharimu Sh. trilioni 6.65 utakapokamilika miaka miwili ijayo, Waziri January anasema matarajio ni kupatikana umeme wa kiwango cha MW 2,115, ambacho ni sawa na asilimia 136 ya uwezo wa uzalishaji umeme nchini kwa sasa. Kwa lugha rahisi, mara mbili ya umeme unaopatikana nchini na ziada ya theluthi moja.

Anaeleza wasifu huo kwamba manufaa yake mbali na kutosheleza mahitaji ya umeme kitaifa ikiwamo miradi mikubwa kama reli ya kisasa (SGR) inayotumia umeme mkubwa, pia utauzwa nje kwenye nchi jirani.

Hapo Waziri Januari anataja baadhi yake, mataifa Zambia, Burundi na Rwanda ambayo pia ni wadau wakubwa wa Tanzania kwa bandari zake huku Zambia ikiwa na ubia wa zaida wa reli ya TAZARA, vivyo hivyo mradi wa reli ya kisasa inazihusu moja kwa moja nchi za Rwanda na Burundi.

Kwa mujibu wa Waziri January ambaye huko nyuma kabla ya kuwa waziri, alishaongoza Kamati ya Bunge inayoshughulika na nishati, anasema mradi huo ni wa nne kwa ukubwa





## TOLEO MAALUM

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO





barani Afrika, kwa Afrika Mashariki wenyewe ndiyo mkubwa zaidi.

Hapo Waziri January anajivunia manufaa yake kwamba: "Kukamilika kwa mradi huu kutapelekea kuwa na umeme wa uhakika zaidi nchini na hivyo kuchangia katika Pato la Taifa."

SIRI YA MAFANIKIO

Ufanunuzi uliotolewa kwa mashuhuda ambao Nipashe ni sehemu yao katika mradi huo wa uzalishaji umeme, ni kwamba wakati katika miaka miwili ya utekelezaji wa mradi ulifanikishwa kwa asilimia 37 ya malengo, ndani ya mwaka mmoja uliopita kazi ya mradi imetekelezwa kwa asilimia 30 na kufanya jumla ya utekelezaji kuwa wa asilimia 67.

Hapo likaibua swali aliloelekezewa moja kwa moja Mwenyekiti wa Kikao cha Ufafanuzi, Waziri January ambaye naye kwa mara ya kwanza ameamua kuwa wazi kuanika mambo makuu mawili yaliyo nyuma ya pazia.

Hapo anaanika siri uteuzi wake kwenye dhamana aliyonayo sasa, imeendana na sharti toka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwamba 'asimzunguke' kwenye kufanikisha mradi huo, hali inayofanya hatua zake za kiutendaji ziwe 'mguu kwa mguu' na utekelezaji wa mradi huo.

La pili, anaimwagia sifa Bodi mpya ya TANESCO ambayo imekuwa makini sana kwa kila jambo na hali inayohusu kufanikisha mradi huo, leo hii ukitoa matunda chanya.

Waziri January anasema mambo hayo mawili ya kiutawala, yamekuwa yakiendana na hatua kiserikali kuelekeza fedha zinazotakiwa kwenye mradi, nayo ikiuweka mbali na hatua zote za kusuasua, bali kukimbizana na ratiba.

Eneo mojawapo analolitumia kama mfano, kazi za mradi huo zinafanyika kwa saa 24 siku zote za juma na hata sikukuu, jambo linaloibua ufanisi mkubwa.

Nipashe iliyokuwapo kwenye mradi siku ya maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima, maarufu Nanenane, ilishuhudia tarehe hiyo ya mapumziko kitaifa kazi zikiendelea kama kawaida katika vita vya kupigania kufikia lengo la mradi kuanza kutumika Aprili 2024.

"Tangu bodi na menejimenti hii imeingia, tumeridhishwa sana na usimamizi wa mradi huu," anasema Waziri January na kusisitiza usimamizi huo aliouita wa kisayansi, akiwa na ufafanuzi wamezingatia ratiba na usimamizi wa fedha za umma, umefanya utekelezaji wa mradi kuwa wa kasi zaidi na utakapokamilika utakuwa katika ubora.

Mabadiliko hayo makubwa ndani ya TANESCO yalifanyika Septemba 25 mwaka jana, Rais Samia alipomteua Chande kuwa Mkurugenzi Mkuu akichukua nafasi ya Dk. Tito Mwinuka na Omari Issa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya shirika hilo.

Waziri January anaendelea na ufafanuzi: "Huu ni ushindi na wenye faraja kwa kufikia hatua hii kubwa. Unajua hizi kazi si kupiga siasa tu, kazi kubwa imefanyika ndani ya mwaka mmoja, si kila kitu ni cha kusema ila matunda ya ukimya na kupiga kazi ndiyo haya.

"Kwa sasa tumefika asilimia 67, katika miaka miwili na nusu ya mwanzo (kuanzia Desemba 2018 - Juni 2021) tulifikia asilimia 37. Leo tuko asilimia 67, ni kasi kubwa katika kipindi hiki kifupi.

"Sasa hivi hapa kazi inafanyika saa 24, hakuna mapumziko, leo ni sikukuu ya Nanenane lakini kazi inaendelea hapa, yaani ni saa 24 siku zote za wiki na hata siku za sikukuu, kwa hiyo kasi imeongezeka."

Waziri January anaongeza kuwa katika kipindi hiki cha uongozi wa serikali awamu ya sita, kumeshuhudia kasi zaidi katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati.

Waandishi wa habari walipohoji lini wataanza kujaza maji kwenye bwawa hilo, Mhandisi Mkazi wa mradi huo, Mwandambo, alikuwa na mrejesho kwao, akisema: "Kujaa kwa bwawa kunategemea mvua lakini misimu miwili inatosha au mmoja ukiwa na mvua kubwa".

Katika ziara yake hiyo, Waziri January alitembelea na kukagua kila kitengo cha mradi huo ili kuangalia hatua mbalimbali zilizofikiwa.

**UPEKEE WA MRADI**

Umbali kutoka uliko mradi huo wa umeme kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam, ukifananishwa kwa mtazamo wa ramani na umbali rasmi wa barabara kutoka Dar es Salaam na Mji wa Morogoro, kwa ujumla inafanana.

Hata hivyo, kwa anayesafiri kati ya Dar es Salaam na Morogoro kwa basi dogo ni wastani wa saa tatu na nusu hadi nne, lakini safari hiyo kutoka jijini hadi kwenye mradi wa umeme, kwa kutumia usafiri huo huo, inamchukua abiria saa 11.

Hapo ina maana usafiri ule ule, barabara hiyo hiyo ya Dar es Salaam-Morogoro, abiria anatumia wastani au zaidi ya theluthi mbili ya kwenda Morogoro kisha anachepuka kushoto kuingia eneo la Ngerengere mkoani Morogoro ambako anaendelea na barabara iliyotawaliwa na vumbi jekundu lenye utamaduni wa kuunda tope na vipande vichache vyenye lami hadi kwenye mji mdogo wa Kisaki mkoani humo.

Hapo ndipo anapoanza kuingia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na masharti yaliyoko huko ni kuendesha chombo cha moto kwa kasi maalum iliyowekwa kisheria, inamchukua saa tatu kufika kwenye mradi.

Katika mustakabali huo, ushuhuda wa Nipashe ziarani ukioanishwa na ufafanuzi wa kiutawala kuhusu miundombinu ya mradi, unaanika sababu na uhalisia wa mahitaji yake ambayo Mhandisi Mkazi, Mwandambo, anaiorodhesha katika mambo manane yanayotekelezwa.

Katika saa 24 za ushuhuda huo, ilionekana shughuli za ujenzi wa barabara ukiendelea na kazi, daraja likiwa limeshaanza kutumika wakati wakimalizia ujenzi wake na malori yenye mizigo toka wilaya jirani yakikatiza.

Sura nyingine iliyoshuhudiwa mahai huko inafanana na aina fulani ya maonyesho kwa maana kundi kubwa la watumishi waliogawanyika katika vitengo vya kila mmoja na jukumu lake, akiwajibika katika nafasi yake kuanzia kwenye mitambo hadi ofisini.

Hata hivyo, kwa muda huo ambao Nipashe ilikuwapo mahali huko, ilibaini katika sehemu kuu za ujenzi wa mradi, kwa kiasi kikubwa watendaji walikuwa kundi kubwa la vijana wakifuatiwa na wachache wenye umri wa kati, ambao wengi wao ni wanaume, kinamama wakipatikana zaidi katika shughuli za ofisi na huduma zingine za kiutendaji.

Katika kinachoendana na kauli ya Mhandisi Mkazi Mwandambo, asilimia kubwa ya watendaji ambao jumla ya 12,000, ni Watanzania huku Nipashe ikishuhudia wachache ambao ni wageni, ikidokezwa kwamba jumla yao haizidi asilimia 10.

Upande wa vifaa, hapo ndipo kukawapo ushuhuda unaoutofautisha mradi huo na mingine mikubwa iliyozoeleka sehemu nyinginezo kama vile kwenye Bandari ya Dar es Salaam na nyinginezo, huko kuna mitambo na mashine zenye uwezo wa ziada wa kuinua mizigo mizito.

Katika hilo, Waziri January ana simulizi zenye ufafanuzi kuna mashine kwenye mradi huo zina uwezo wa kubeba mzigo wenye uzito wa hadi tani 400 na hata kufikishwa katika eneo hilo la kazi kutoka nje ya nchi ilikoagizwa, kulifanyika utaratibu maalum wa kusafirisha kwa njia ya treni na mengine mengi ya kifundi ya ziada kuwezesha kuifikisha.





Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Chonde chonde madereva epukeni vilevi

**SIKU** za hivi karibuni kumetokea mfululizo wa matukio ya ajali za barabarani kwa kupoteza maisha ya watu wengi na wengine kuachwa na majeraha au ulemavu wa kudumu.

Matukio hayo ya ajali baadhi yanasababishwa na mwendo kasi na uzembe wa madereva kutozingatia alama za barabarani.

Pia baadhi ya madereva kugundulika kwenye magari yao kuwa na vilevi hali inayoonesha kuwa wanaendesha huku wakitumia vilevi hivyo.

Utumiaji wa vilevi ukiwa unaendesha gari lazima utaleta madhara kwa sababu dereva anashindwa kudhibiti ajali inapotokea kutokana na kutokuwa na umakini.

Kilevi kinapotumika hata kwa mtu anayetembea kwa miguu kinaonekana kumyumbisha na kukosa mwelekeo wa kule anakoelekea na gari hivyo huwa mbaya zaidi kwasababu ya kasi ya chombo kushindwa kukidhibiti.

Pamoja na madereva kukemewa kuhusu tabia hiyo, lakini baadhi wanaonekana kupuuza na kuendelea kupoteza maisha ya watu wasiokuwa na hatia.

Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa, limeamua kuwaonya madereva wa vyombo vya moto kujihusisha na matumizi ya pombe wawapo barabarani.

Akitoa onyo hilo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Noah Mwakyoma, alisema mkoa wa Iringa umejipanga kukabiliana na ajali za barabarani kwa kuwadhibiti madereva wenye tabia hiyo.

Akitaja sababu mbalimbali zinazochagiza kuongezeka kwa ajali za barabarani anasema ni pamoja na matumizi ya pombe na dawa za kulevya kwa madereva wakati wakiwa wanaendesha vyombo vya moto.

Anasema wako baadhi ya madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani na wakati mwingine makosa yao husababisha ajali na kukatisha uhai wa watu na wengine kupata ulemavu wa kudumu kitu ambacho hakikubaliki.

Mkakati uliowekwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Iringa ni kuwachukulia hatua za kisheria madereva wote watakaobainika kukiuka sheria za usalama barabarani ili iwe funzo kwa wengine wenye tabia hiyo.

Kadhalika, jeshi hilo linaendelea kuwapima madereva kabla ya kuanza safari ili kupunguza ajali za barabarani zitokanazo na ulevi na kuwachukulia hatua wale wanaobainika.

Madereva wanaotajwa zaidi kutumia vilezi wakati wanapokuwa kwenye vyombo vya moto ni wanaoendesha bodaboda na bajaji.

Vile vile, madereva hao wanakiuka viwango vya kubeba abiria wanavyotakiwa kwenye vyombo hivyo kwa kuongeza idadi.

Kwa mfano pikipiki inatakiwa kubeba abiria mmoja, lakini baadhi ya madereva hupakiza abiria wanne pamoja na dereva idadi inakuwa watu watano sawa na gari ndogo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, takriban watu 1,191 walifariki dunia na 2,139 kujeruhiwa kutokana na ajali za barabarani 1,594 zilizotokea nchini kati ya Julai mwaka 2021 na Machi mwaka 2022.

Idadi hii ya vifo ni kubwa na ukiangalia baadhi yao wameacha familia ambazo zilikuwa zikiwategemea.

Baadhi ya watu wamepoteza familia nzima na kuachwa wapweke na wengine kuwa na ulemavu wa kudumu.

Ni jukumu la madereva, abiria kuwa makini wanapokuwa barabarani. Abiria wana haki ya kumwonya dereva anapoonekana kufanya vitendo vitakavyosababisha ajali.

Elimu pia inatakiwa kutolewa mara kwa mara na ufuatiliaji kwa madereva ili kudhibiti ajali. Wananchi ni wajibu wao kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwasababu wao ndiyo waathirika wakubwa zinapotokea ajali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Anthony Gervas

## Muungwana Lazima Nilonge

# Migogoro hii ya vyama inanyonga demokrasia

**SIASA** za makundi ndani ya vyama bado zinaendelea kujitanua na kupata nafasi hasa miongoni mwa viongozi wakuu na nyakati za kugombea nyadhifa mbalimbali ndipo changamoto zinapoonekana zaidi.

Ninajiuliza kwanini viongozi wa chama waendelee kuruhusu mipasuko ya makundi kuanzia wanachama hadi viongozi, hasa unapofika wakati wa kugombea uongozi wa ngazi mbalimbali kuanzia kwenye mashina hadi mikoa.

Hapo ndipo, utaona viongozi wanaopaswa kusimamia wanashindwa kuhakikisha kuwa kunakuwapo na siasa bora zenye kundi moja au kupata viongozi watakaoweza kukivusha na kusonga mbele katika utekelezaji wa ilani baada ya uchaguzi.

Kuwapo kwa makundi, fitina, majungu, kuchafuana wenyewe kwa wenyewe iwe wanachama, viongozi au wagombea, kadhalika ubaguzi wa kijinsia, minong'ono ya ukabila, ukanda na udini vyote vinasababisha mpasuko, mgawanyo na makundi ndani ya vyama.

Wanachama wanaosababisha yote hayo ni wale wenye tamaa ya madaraka, au wanaotumiwa na maadui kuviangusha vyama vyao au wanaoamini kuwa ndiyo wenye nguvu wakitaka wapishwe na wale wanyonge.

Inawezekana ni nguvu ya pesa za kuwajaza wanachama waliozoeshwa hivyo na baadhi ya viongozi au wagombea wakati wa uchaguzi au hata kutumiwa na maadui ili kukivuruga chama.

Ukitaka kupata majibu yake bila kificho ni nyakati za uchaguzi ndani ya chama, au kampeni zinapoanza, ukitumika msamiati kwamba wao hawashindani bali wanapanga na kuchagua uongozi wanavyoona au kutaka.

Matatizo yanaibuka wakati wa kuanza mchakato wa uchaguzi kwenye serikali za mitaa, vitongoji na wenyeviti wa vijiji dhidi ya wapinzani wao.

> **Tatizo la rushwa nalo ni miongoni mwa ugonjwa unaochangia mipasuko na makundi na migawanyiko mbalimbali ndani na nje ya vyama.**

Hali kadhalika, wakati wa uchaguzi mkuu kwenye nafasi za madiwani, wabunge na hata Rais. Ndiyo muda wa kutoana jasho wagombea wakianza kulizwa kwenye kura za maoni na wakati mwingine hata kutishiana vikali, huku wengine chuki zikitawala mioyoni na kushindwa kusalimiana.

Tatizo la rushwa nalo ni miongoni mwa ugonjwa unaochangia mipasuko na makundi na migawanyiko mbalimbali ndani na nje ya vyama.

Mfano, mkoani Mwanza hivi karibuni kumekuwapo na uchaguzi lakini katika baadhi ya maeneo zimeripotiwa figisu na pengine kura zinapigwa hata usiku.

Kuna sehemu uchaguzi ulifutwa kutokana na wagombea wengine kudai kuwa wenzao wameteuliwa badala ya kuchaguliwa na kuhoji sababu ya viongozi kujipangia safu za wanaowataka badala ya kufanyika uchaguzi kama katiba na sheria zinavyoelekeza.

Leo, CCM imetimiza miaka 45 tangu kuzaliwa mwaka 1977, kikiwa ni chama kikongwe bado wanachama wake baadhi wanadaiwa kufanya siasa kwa utaratibu wa bora liende, kama ilivyotokea Mwanza.

Huenda ndiyo sababu Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa, alianzisha vyuo vya siasa ili watu wajifunze siasa bora zenye manufaa kwa chama.

Swali langu kwa wenye vyama ni hili, hivi siasa za makundi na kusalitiana zitaisha lini? Sitaki kuzungumzia yanayotokea CUF wala NCCR-Mageuzi, lakini ni lini mabadiliko yatakuja ili kuwapata viongozi bora badala ya bora viongozi wanaolelewa na kukuzwa na migogoro isiyokwisha?

Migogoro mingi inaripotiwa kwenye vyama na kinachoonekana ni baadhi ya wanachama na viongozi kuwa madalali wa kutafuta fedha ili kujinufaisha.

Rais Samia Suluhu Hassan, ameruhusu demokrasia kuchukua mkondo wake katika vyama vyote ya siasa lengo ni kuleta mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kuondoa itikadi za kibaguzi ndani ya vyama na kuwa na mazingira yanayowapa Watanzania haki ya kushiriki siasa kwa amani, lakini vyama havijatulia na kutumia fursa hiyo.

Ni wakati wa kubadilika na kuwang'oa viongozi wasioleta mabadiliko bali migogoro ndani ya vyama na kusababisha mipasuko na makundi yanayoharibu sifa za vyama.

# Intaneti Kilimanjaro kuipaisha Tanzania kimapato, ujio watalii

Na Waandishi Wetu

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, amesema uwapo wa mawasiliano ya intaneti katika Mlima Kilimanjaro kutaiongezea nchi mapato na kuitangaza duniani kwa watalii kurusha mubashara wanavyotembelea kivutio hicho.

Nape alisema hayo jana katika kituo cha utalii cha Horombo kilichoko umbali wa mita 3,720 usawa wa habari, wakati wa uzinduzi wa intaneti kwenye mlima huo ambao haukuwa na huduma ya mawasiliano.

"Mara kadhaa nimesikia katika malango ya kuingia katika hifadhi na vivutio vya utalii wageni wanatumia muda mrefu kujisajili kutokana na mtandao kuwa chini, hili siyo sawa nategemea tutaondoa matatizo hayo, mtandao utapatikana,"alisema.

"Kwa uzinduzi wa intaneti hii sasa watalii wanaweza kupiga picha za mnato, video na mawasiliano mengine ya simu kwenda nchi mbalimbali duniani. Hii itaboresha sekta ya utalii, tuendeleze uboreshaji huu hadi kilele cha Uhuru kilichoko umbali wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari," alisema.

"Hii ilikuwa hatari kwa usalama wa watalii na watoa huduma za watalii, serikali ilikuwa inakosa mapato sambamba kuwanyima watalii kutangaza matukio mbalimbali ya utalii wakiwa Mlima Kilimanjaro " alisema.

Waziri Nape alisema watalii na watoa huduma watapata huduma ya mawasiliano katika vituo ndani ya mlima huo, ambavyo ni Mandara, Horombo, Kibo na kilele cha Mlima Kilimanjaro (Uhuru Peak).

"Tumekusudia na ninashukuru Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kwa uamuzi huu, leo tunazindua hapa kabla ya mwisho wa mwaka nimeambiwa kwa huduma hii itakwenda kuwahudumia watalii na watoa huduma za kitalii kati ya 800 hadi 1,000 kwa siku," alisema.

Waziri Nape alitoa rai kwa TTCL kuhakikisha huduma zinapatikana kwa urahisi na uhakika na kueleza kuwa kuimarika kwa mawasiliano ya intaneti katika Mlima Kilimanjaro kutaleta maendeleo makubwa kwa taifa.

Alisema mawasiliano hayo yatarahisisha juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kukuza utalii kwa kutengeneza mazingira mazuri na rafiki kwa watalii kupata huduma hiyo kupitia filamu ya Royal Tour.

"TTCL ina huduma ijulikanayo kama 'fiber mlangoni mwako' ambayo inalenga kufikisha huduma za mawasiliano ya intaneti katika makazi ya wananchi na maofisini, hii ndio dhamira ya serikali inayoongozwa na Rais Samia," alisema.

Nape alisema huduma hiyo ni nzuri na bei za data zimeshuka na kuielekeza Wizara ya Habari kuharakisha mchakato ili kuwakabidhi mkongo kwa TTCL ili wauendeshe.

"TTCL mhakikishe huduma zinapatikana na mnakagua mara kwa mara huduma zenu na njia za mawasiliano ya mkongo ili tupunguze malalamiko yasiyo na tija, harakisheni miradi yote ya maboresho ya mkongo wa taifa inakamilika kwa wakati,"alisema Nape.

**Imeandikwa na Romana Malya (DAR) na Mary Mosha (MOSHI)**

# Shaka awa mbogo mtendaji kudaiwa kutafuna fedha za ujenzi wa vyoo vya shule

**Na Beatrice Shayo,** KALIUA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ameagiza kuchukuliwa hatua kwa aliyekuwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ibambo, Kaliua mkoani Tabora, Adam Mnyaga, kwa madai ya kula Sh. 950,000 za michango ya wananchi kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya shule.

Kadhalika, Shaka amezitaka halmashauri kuacha mtindo wa kuwalea viongozi wa vijiji ambao ni wabadhirifu na kuwasababishia wananchi kuteseka.

Shaka aliyasema hayo jana mjini hapo wakati akikagua ujenzi wa jengo la Hospitali ya Mwongozo huku akibainisha kuwa haiwezekani kiongozi aliyekula fedha za michango halafu anahamishiwa kijiji kingine.

"Tusiwafanye wananchi ni ng'ombe wa maziwa, hii si sawa kabisa. Wananchi wanataka fedha zao kwa ajili ya maendeleo halafu anajitokeza mjanja mmoja anaondoka. Hii si sahihi na ni kuwaumiza wananchi," alisema.

Tumeshamwagiza mkuu wa wilaya na mkurugenzi wa halmashauri inakuwaje mtu anaharibu halafu anahamishiwa sehemu nyingine. Ameharibu sehemu moja anachukuliwa akaharibu sehemu nyingine kuwaumiza hawa wananchi. Hii haiwezi kukubalika," alisema.

Baada ya kutoa maelezo hayo, Shaka alimtaka msaidizi wa mkurugenzi, Kennath Tefumkwa, kutoa maelezo kuhusiana na suala hilo alieleza walivyopatiwa hiyo kesi alihamishwa na kupelekwa katika kijiji kingine kwa ajili ya kupisha uchunguzi.

"Kama amekula hela za wananchi na ofisi imejiridhisha, kwa nini wamemhamisha kwenda kijiji kingine jamani. Hii ni sahihi taarifa tulizo nazo ofisi ya Mkurugenzi inalaumiwa, tunayo orodha ya watendaji ambao ni wabadhirifu katika halmashauri hii," alisema.

Alisema CCM haiwezi kuvumilia watendaji ambao wanawalea wabadhirifu wanawachonganisha wananchi na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anawaza kila kukicha namna ya kuwakwamua wananchi kiuchumi.

Aidha, alisema kiongozi huyo anatakiwa kulipa fedha za wananchi na kuchukuliwa hatua za kinidhamu za kutumishi amesababisha uhaba wa choo na kusisitiza kwamba serikali haitamvumilia mbadhirifu yeyote awe kwenye kijiji, kata, wizara, halmashauri ama mkoa.

Katika hatua nyingine, Shaka alielezea kukerwa na tabia ya fedha za miradi ya maendeleo kucheleweshwa kwa kisingizio cha mifumo ulipaji kutofunguka. "Msitumie mfumo kama kisingizio cha urasimu kukwamisha shughuli za wananchi tunakwenda kufuatilia tuambiwe shida ni nini haiwezekani mfumo uwe mwezi mzima haufunguki mimi siwaelewi na siamini mfumo haufunguki mwezi nzima hata siku moja nitaenda kufuatilia kwa nini kumekuwa na urasimu kwenye masuala muhimu na ya msingi yanayogusa hawa wananchi," alisema.


**TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC)**

**Re- Advertisement**

**CALL FOR CONCEPT NOTES FROM POTENTIAL INVESTORS FOR THE DEVELOPMENT AND OPERATION OF A COMMERCIAL BUILDING AND TOURISM INVESTMENT AT KIMANDOLU IN ARUSHA**

1. The Government of the United Republic of Tanzania, through the Tanzania Investment Centre (TIC), has allocated 47,324 square metres of land for investment in commercial building and tourism investment development opportunity at the Kimandolu, Arusha site.
2. Kimandolu is located approximately 5 Km from Arusha City centre, accessible through old Moshi tarmac road and it is situated alongside the Old Moshi Road. With ideal tourism climatic conditions, high demand of commercial building infrastructure and tourism facilities, Arusha City is well positioned to serve the growing demand of tourist hotel beds, residential apartment and office accommodation demand-supply gap in the Northern tourist/ Commercial circuit.
3. Through the Tanzania's five years strategic development plan initiative commercial developers do also stand to gain from complimentary investments opportunities by private investors in infrastructure, and tourism sector.
4. Kimandolu investment site for commercial building and tourism investment land allocation process will be guided by the Tanzania Investment Centre approved land allocation manual.
5. TIC is now inviting Concept Notes from Investors/ Developers who are interested to invest in commercial building and tourism investment to submit their concepts notes to invest and develop Kimandolu TIC site.
6. The following investment site is available-Plot No. 144/2/1 Block "GG" situated at Kimandolu in Arusha Municipality with 47,324 square meters.
7. The preliminary evaluation criteria for the Concept Notes are as follows:
   i. Quality of the concept note and proposed project/investment;
   ii. Alignment to national priorities: Vision 2025 and the 5-year development plan;
   iii. Value for money in terms of benefits to TIC (including but not limited to land lease rental and concession fee), surrounding community and the Government of Tanzania at large including jobs, government revenues etc;
   iv. Financial capacity for the prospective investor; and
   v. Investor track record or experience in undertaking similar projects; and
   vi. Project development plan, timelines and proposed land lease period.
8. Preferred Developer who meets evaluation criteria will be obtained inline within TIC land bank allocation procedures and guidelines;
9. Applicants who had earlier on submitted their proposal prior issuance of this notice are required to submit their application in-line with this notice requirements;
10. The deadline for Concept Note submission shall be on **Monday 15th September, 2022 at 02:00Pm (EAT).** The hard copy of the proposal should be submitted to

**Tanzania Investment Centre (Head Office),**
**Shaaban Robert Street, 9A & B,**
**P.O Box 938, Dar es Salaam,**
**Tanzania.**

Please note that, late submission will not be accepted.

Proposal must be clearly marked: **Concept Note for commercial building and tourism investment at TIC Kimandolu Arusha Site.**

Further enquiry should be communicated by **E-mail on info@tic.go.tz**

216995801

# Huduma Bolt sasa kwa wanaotumia kadi pekee

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya usafirishaji abiria ya Bolt, imesema kuanzia leo itaanza kutoa huduma kwa wateja wanaotumia kadi pekee.

Meneja wa Bolt Kanda ya Afrika Mashariki, Kenneth Micah, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kampuni hiyo itakavyoendelea kutoa huduma hiyo nchini. Alisema LATRA ilitoa agizo Machi 14, mwaka huu, kuhusu gharama mpya za usafirishaji wa abiria, hivyo walikaa kujadili kwa kina namna ya kuboresha huduma hiyo.

"Madhumuni ya taarifa hii ni kuwafahamisha, kama wadau wetu wakuu kwamba Bolt itakuwa ikifanya mabadiliko ya kiutendaji kuanzia Agosti 17, 2022 (leo).

"Mabadiliko haya yatahusisha kuzuia magari yasitumike kwa abiria wa kawaida bali yatumike tu kwa abiria wa kampuni, yaani wateja wa kadi. Inasikitisha kwamba mabadiliko haya yanaweza kuathiri biashara, lakini Bolt haina njia mbadala ya kukabiliana na hasara katika soko," alisema.

Alieleza zaidi kuwa, itawezekana endapo uboreshaji mkubwa katika mfumo wa biashara kuelekea sekta ya usafirishaji utakuwapo ili kuunda hali ya ushindi pande zote miongoni mwa madereva, wasimamizi wa sekta ya usafiri na abiria.

Micah alisema Bolt na LATRA zimekuwa na mawasiliano na majadiliano ya muda mrefu katika kutatua suala hilo.

"Kwa bahati mbaya, majadiliano yamechukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa na hivyo kutoa shinikizo lisilostahili katika uendelevu wa biashara ya Bolt Tanzania," alisema.



Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan (wa pili kushoto), akizungumza na viongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), baada ya kutembelea kampasi kuu ya chuo hicho Mabibo, Dar es Salaam hivi karibuni. (Wa tatu kushoto) ni Mkuu wa chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT na taasisi za elimu ya juu India kushirikiana

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimesema kimepanga kuanzisha ushirikiano na taasisi za elimu ya juu za India ili kuzalisha wataalamu wengi wazawa katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Akizungumza baada ya mkutano wake na Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema jana kuwa:

"Balozi wa India nchini ameahidi kuisaidia taasisi yetu katika kutuunganisha na vyuo vya nchi hiyo ili tuanzishe ushirikiano utakaoongeza tija kwenye utoaji wa elimu kwa chuo chetu.

"Ushirikiano ambao tunaangalia kuuanzisha na vyuo vya India utakuwa wa kubadilishana wakufunzi na wanafunzi na tunapongeza msaada wa dhati ambao umeonyeshwa na Mheshimiwa Balozi wa kuitangaza taasisi yetu India.

"Mbali na kusaidia taasisi yetu kupata ushirikiano zaidi na vyuo vikuu vya India, Ubalozi wa India nchini umeahidi kutuletea vitabu mbalimbali ambavyo vitawasaidia walimu na wanafunzi katika masomo," alisema.

Mkuu wa NIT, alipongeza kuwa Ubalozi wa India pia umesema utatoa nafasi za udhamini wa masomo kwa wakufunzi na wanafunzi katika kujiendeleza kwenye maeneo ya usafiri na usafirishaji.

"Tumefurahi kusikia Serikali ya India itatoa msaada katika kujiendeleza kimasomo walimu wetu pamoja na wanafunzi katika maeneo maalumu ya usafiri na usafirishaji, hii itatoa tija kwa kuzalisha nguvu kazi bora kwenye miradi yetu ya kimkakati kama vile reli, anga na maji," alisifu.

Alisema mikakati yao ya sasa inajumuisha kuendelea kutoa wahitimu wenye vigezo vya kimataifa ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

"Tupo kwenye mipango mikubwa itakayozalisha wahitimu wenye viwango vya kimataifa vitakavyowawezesha kufanya kazi kwenye miradi mikubwa iliyoanzishwa na serikali katika sekta ya usafirishaji.

"Tumeona kwa miaka ya hivi karibuni serikali imeanzisha miradi mikubwa kama vile reli ya umeme (SGR), mradi wa kufua Umeme wa Julius Nyerere, bomba la mafuta kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga na kuimarishwa kwa Kampuni ya Ndege (ATCL). Kutokana na miradi hii mikubwa ya kitaifa, haitahitaji kuchukua wafanyakazi kutoka nje ya nchi," Prof. Mganilwa alisisitiza.

Alisema, NIT ni taasisi mahiri yenye uwezo wa kutoa mafunzo ya kada mbalimbali za usafiri kwa kutumia teknolojia za kisasa na zenye viwango vya kimataifa.

Prof. Mganilwa aliwataka wazazi na vijana wa Kitanzania kuchangamkia fursa hiyo ya mafunzo kwa kuwa sekta ya uchukuzi inakua kwa kasi na ina uhitaji mkubwa wa rasilimali watu, hivyo kwa kusoma kozi hizo watajitengenezea mazingira mazuri ya kupata ajira na kujiajiri.

# Madereva waonywa matumizi ya kilevi

**Na Martha Sambo,** IRINGA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa, limewaonya madereva wa vyombo vya moto kujihusisha na matumizi ya pombe wawapo barabarani.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Noah Mwakyoma, wakati akizungumza na Nipashe namna mkoa ulivyojipanga kukabiliana na ajali za barabarani.

Mwakyoma alisema ziko sababu mbalimbali zinazochagiza kuongezeka kwa ajali za barabarani iwamo matumizi ya pombe na dawa kwa madereva wakiwa wanaendesha vyombo vya moto.

"Wako baadhi ya madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani na wakati mwingine makosa yao husababisha ajali na kukatisha uhai wa watu na wengine kupata ulemavu wa kudumu kitu ambacho hakikubaliki," alisema Mwakyoma.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Iringa halitasita kuwachukulia hatua za kisheria madereva wote watakaobainika kukiuka sheria za usalama barabarani ili iwe funzo kwa wengine wenye tabia hiyo.

Mwakyoma alisema jeshi hilo limeendelea kuwapima madereva kabla ya kuanza safari ili kupunguza ajali za barabarani zitokanazo na ulevi na kuwachukulia hatua wale wanaobainika.

Katika hatua nyingine, Mwakyoma aliwataka madereva wa bajaji kuzingatia maelekezo wanayopewa ikiwa ni pamoja na kubeba abiria watatu ambao wako kwa mujibu wa sheria.

"Kwa muundo, bajaji inabeba watu watatu lakini madereva wengi wamekuwa wakivunja sheria kwa makusudi kwa kubeba abiria wanne hadi watano. Hatutawafumbia macho watawajibishwa kwa mujibu wa sheria," alisema Mwakyoma.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya madereva, akiwamo Baraka Daniel, walisema wameendelea kuchukua tahadhari zinazotolewa na jeshi hilo lakini bado baadhi yao hawazingatii.

"Niliombe Jeshi la Polisi lisichoke kutoa elimu kwetu madereva maana licha ya kwamba baadhi yetu tunafuata sheria bado wako wachache ambao wanakiuka. Kikubwa ni kukosa uelewa tu na wakati mwingine kupuuza. Ni vyema tukaendelea kupewa elimu ya kutosha," alisema Daniel.

# Madiwani wakwama kupata bima ya afya kwa kukosa vyeti vya ndoa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamekosa bima za afya ya NHIF baada ya kukosa vyeti halali vya ndoa ambavyo vingewawezesha kukidhi vigezo vya kuingia kwenye mfumo wa kupata matibabu kupitia bima hiyo.

Wengi wao wamebainika kuwa na vyeti vya ndoa vya kimila ambavyo vinawawezesha kumiliki mke zaidi ya mmoja huku kati ya madiwani 26 ni sita pekee waliofanikiwa kuwa na vyeti halali vya ndoa vinavyotambulika kisheria na kupata bima ya afya.

Hayo yalibainishwa jana katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri hiyo cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022 kilichojadili masuala mbalimbali ya maendeleo na kumthibitisha Diwani wa Kata ya Mwalugulu, Flora Sagasaga kuwa makamu mwenyekiti.

Diwani wa Lunguya, Benedictor Manwali, aliomba Ofisi ya Katibu Tawala wa wilaya kuwalegezea masharti ikiwamo kuvitambua vyeti vya ndoa za kimila ili kuwawezesha kupata bima hiyo na kuchangia asilimia tatu ya sehemu ya posho yao ya kila mwezi.

Alisema, kati ya madiwani waliopo halmashauri hiyo madiwani wawili pekee wenye ndoa halali, waliosalia hawana vyeti vya ndoa na kufanya zoezi la upatikanaji wa bima hizo kuwa mgumu kwa upande wao.

Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma, alisema ni mara ya pili madiwani kutangaziwa bima hiyo kujiunga na walishindwa kukidhi vigezo kutokana na sababu hizo hizo.

Alidai kuwa, ili kufanikiwa zoezi hilo na kila diwani awe na bima ya afya, serikali inatakiwa kutambua vyeti vya ndoa vya kimila ambavyo ni rahisi kuwa navyo.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Charles Fussi alisema, atawachangia asilimia tatu madiwani watakaokidhi vigezo vya kupata bima hiyo na kuwataka wasiokuwa na ndoa kufunga za Bomani ili kuwawezesha kuwa na kigezo.

Akijibu hoja hiyo Katibu wa Bima ya Afya ya NHIF Halmashauri ya Msalala, Ignasi Lufulila, alisema ili diwani aweze kupata bima hiyo anatakiwa kuchangia asilimia tatu ya posho yake ya kila mwezi na mwajiri wake ambaye ni Mkurugenzi kuchangia pia kiasi hicho na kila diwani ana kigezo hicho.

Alisema, moja ya kigezo kinachosababisha madiwani kutokupata bima ni ukosefu wa vyeti vya ndoa na wengi wao wanandoa za kimila ambazo serikali haivitambui na inatambua vyeti vinavyotolewa katika madhehebu mbalimbali ya kidini na Bomani pekee.

Mmoja wa maofisa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini, aliwataka madiwani wanaohitaji kupata ndoa za bomani kujiorodhesha majina yao kama walivyofanya madiwani wa Ushetu na watawafikia kuwafungisha ndoa baada ya kutangazwa majina yao kwa siku 21.

Alisema, hata kama kuna diwani atakuwa na mke zaidi ya mmoja, atafungishwa ndoa kulingana na wake alionao, kwa kuwa sheria inawataka pia kuwafungisha ndoa wenye wake wengi ili mradi siku hiyo ataambatana nao wote na kila mmoja atapewa cheti halali cha ndoa na watakuwa na uwezo wa kupata bima za NHIF.

## Madereva wapewa mwezi kutumia kituo cha Mafiga

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MADEREVA wa mabasi ya abiria yanayofanya safari zake wilayani na ndani ya mji wa Morogoro wamepewa mwezi mmoja kupakia na kushusha abiria ndani ya kituo kipya cha Mafiga mjini hapo.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Paschal Kihanga, alisema hayo katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani Manispaa ya Morogoro na kubainisha kituo hicho kimegharimu mamilioni ya fedha na hakipaswi kutotumika.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa hiyo, Ally Machela, kuhakikisha anasimamia utekelezaji wa maagizo hayo na kuwachukulia hatua wale wote watakaokiuka utaratibu huo.

Kihanga alisema tangu kuhamishwa kwa mabasi kutoka katikati ya mji ili kupunguza foleni na kuhamia Mafiga, manispaa hiyo inapoteza mapato kutokana na daladala kushindwa kufika kituoni hapo kwa kuishia njiani kwa kukwepa ushuru.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Wakili Albert Msando, alisema wamesajili askari 50 wa jeshi la akiba, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoani Morogoro kwa ajili ya kudhibiti mabasi yanayoshindwa kufika Mafiga.

Msando alisema imetosha kuacha upotevu wa mapato yanayosababishwa na daladala na bajaji kukwepa ushuru na kwamba ni lazima yakusanywe na kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aliwataka madiwani kusimamia miradi ya maendeleo katika kata zao ili hata wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru iwe rahisi kuchagua miradi yenye ubora unaokubalika.

"Kwenye hili la kusimamia mapato hatutafumbia macho watendaji wanaozembea, fedha hizi zinategemewa kusaidia maendeleo ya wananchi ni lazima usimamizi uwe madhubuti, mbaya zaidi watendaji wengine wanashindwa kusimamia miradi na kuandika kabisa haifai kuzinduliwa na Mwenge, halafu ndiyo uwafae wananchi? Hapana," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Morogoro Mjini, Fikiri Juma, aliwataka madiwani kuendelea kushirikiana na watendaji kuhakikisha mapato ya halmashauri hiyo yanakusanywa kwa ufanisi na tija.




Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando (wa pili kulia), akiwa na Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Kati, Joseph Sayi (kulia), baada ya kuwakabidhi zawadi washindi wawili waliojishindia bodaboda kupitia promosheni ya Vodacom "M-Pesa Imeitika", mjini Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama kutoa uamuzi mshtakiwa aliyetoroka akiwa nje kwa dhamana

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Agosti 18, 2022 inatarajia kutoa uamuzi wa dhamana kwa Meneja wa Kampuni ya Sanitary Appliance and Hardware Ltd, Hasnei Mawji (39), anayetuhumiwa kutoroka kwenye kesi ya jinai 373/2018 akiwa nje kwa dhamana.

Mawji, Festo Kasasa (55) na Hassan Amirali (49), Msimamizi wa kampuni hiyo, wanadaiwa Januari 11, 2018 katika Jiji la Dar es Salaam walikula njama ya kuiba vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 181.9.

Wakili wa Serikali, Coroline Materu, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ritha Tarimo, kuwa wameshawasilisha viapo mahakamani hapo kama mahakama ilivyoelekeza kutokana na kupinga Mawji asipewe dhamana.

Kutokana na upande wa mashtaka kukamilisha viapo hivyo, Hakimu Tarimo aliahirisha kesi hiyo hadi kesho kwa ajili ya uamuzi kama mshtakiwa atapewa dhamana.

Awali, mshtakiwa huyo anadaiwa kutoroka dhamana katika kesi ya jinai namba 373/2018 iliyokuwa inamkabili yeye na wenzake wawili katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala.

Hali hiyo ilisababisha Wakili Materu kuiomba mahakama hiyo izuie dhamana ya mshtakiwa huyo, kutokana na kutoroka dhamana kwenye kesi ya Mahakama ya Ilala.

Mawji, Kasasa ambaye ni dereva mkazi wa Majohe na Amirali, msimamzi wa kampuni hiyo, wanadaiwa Januari 11, 2018 katika Jiji la Dar es Salaam walikula njama za kutenda kosa.

Inadaiwa siku na eneo hilo washtakiwa kwa pamoja, wakiwa watumishi wa kampuni hiyo, waliiba vitu mbalimbali ikiwamo nyaya ambazo hazishiki kutu zenye thamani ya Sh. 181,985,000.

# Tril. 1.1/- kufikisha maji Dar na Pwani

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imetenga Sh. trilioni 1.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira Dar es Salaam na Pwani pamoja na shughuli mbalimbali za uendeshaji na uboreshaji wa utoaji wa huduma.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki kwenye ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za DAWASA kwa mwaka wa fedha 2021/22, pamoja na kuelezea mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema kuwa lengo la mamlaka kufanya uwekezaji huo ni kuhakikisha huduma ya majisafi kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani inapatikana kwa asilimia 100 ifikapo 2023.

Aliongeza kuwa kwa sasa upatikanaji wa huduma ya majisafi umeimarika kwa kiasi cha asilimia 96 kwa Dar es Salaam na Pwani na kupitia mpango biashara unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2021/22 - 2023/24).

Alisema mamlaka imejiwekea malengo ya kuhakikisha huduma ya majisafi inapatikana kwa asilimia 100 pamoja na huduma ya usafi wa mazingira inaboreshwa kufikia asilimia 60 katika eneo lake la huduma.

"Tumefanikiwa kutoa huduma kwa asilimia 96, hivyo tuko mbele ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inayoelekeza upatikanaji wa huduma ya majisafi ifikapo 2025 uwe asilimia 95 kwa mijini na asilimia 85 kwa vijijini," alisema Mhandisi Luhemeja.

Pia mafanikio hayo yametokana na kazi kubwa iliyofanywa na mamlaka kupitia wahandisi wake wa ndani ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo upanuzi wa mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Chini.

Alitaja ujenzi wa mtandao wa mabomba wa kilomita 4,700 na ujenzi wa matangi ya kuhifadhi maji kwenye maeneo mbalimbali ya huduma.

Aidha, alisema kazi hiyo imechochea kuongezeka kwa idadi ya wateja kutoka 217,766 mwaka 2018 hadi kufikia 370,982 mwaka 2022.

Alibainisha kuwa miradi ya kimkakati iliyotekelezwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi ni pamoja na mradi wa kusambaza maji Makongo hadi Bagamoyo, Jeti - Buza, Mkuranga, Pugu - Gongo la Mboto, Kibamba - Kisarawe, Mlandizi - Chalinze - Mboga, Mbwawa, Soga na Zegereni.

Alitaja miradi mingine kuwa ni ya uboreshaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuboresha huduma kwa wateja na kupunguza gharama za uendeshaji.

Baada ya kukamilika kwa miradi hii ya majisafi na usafi wa mazingira, kazi itakayobaki itahusisha usogezaji wa huduma kwa wananchi kwa kufanya maunganisho.

"Kwa mwaka huu wa fedha 2022/23, DAWASA inakusudia kuanza utekelezaji wa mradi wa Bwawa la Kidunda ambapo mwezi Oktoba mkandarasi ataanza kazi rasmi. Mradi huu wa kimkakati utasaidia kuongeza upatikanaji wa maji kwa Dar es Salaam na Pwani kwa asilimia kubwa na kuweka uhakika wa upatikanaji wa maji kwa kipindi chote cha mwaka," alisema.

Alitaja mradi wa Rufiji unaotarajiwa kuzalisha lita milioni 750 za maji kwa siku, utatekelezwa na kuongeza maradufu uhakika wa maji kwa Dar es Salaam na Pwani.




Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti (kulia), akitoa ishara ya kuzindua kampeni ya kuhamasisha utalii wa ndani kwa kupanda Mlima Kilimanjaro kwa wafanyakazi 28 wa kampuni hiyo, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya programu za kujenga afya ya mwili kwa wafanyakazi wake kupitia kufanya mazoezi ambapo wakitarajiwa kushuka Jumamosi Agosti 20. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wawafukuza watumishi 4 wa h'shauri

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga limewafukuza kazi watumishi wanne wa halmashauri hiyo kwa makosa ya uzembe na kumsababishia mwajiri wao hasara ya Sh. milioni 40.

Akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne cha mwezi Aprili hadi Juni, 2021/2022, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mibako Mabubu alisema, wamefikia uamuzi huo baada ya baraza hilo kujigeuza kuwa kamati na watumishi hao kufikishwa mbele ya kamati na kupatikana na makosa.

Mibako alisema watumishi hao walifanya uzembe na kumsababishia mwajiri hasara, pamoja na kukiuka maadili ya utumishi wa umma na taratibu zake.

Watumishi waliofukuzwa kazi ni Edward Masatu Mnyoro aliyekuwa Mwekahazina, Dk. Ntanwa Kilagwaye, daktari wa mifugo na Sheila Chaula, ofisa mahesabu ambao wamekwenda kinyume na maadili ya utumishi wa umma kwa kufanya ubadhirifu wa Sh. milioni 35.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Buruma, Lazaro Mohamed, aliyekuwa anasimamia ujenzi wa Zahanati ya Matinje, anadaiwa kukiuka maadili ya utumishi wa umma kwa kufanya uzembe na kumsababishia mwajiri wake hasara ya Shilingi milioni tano.

Mibako alisema mtumishi yeyote asiyeridhika na maamuzi hayo, haki ya rufani iko wazi na wanatakiwa kurudisha fedha hizo Sh. milioni 35 na Shilingi milioni tano.

Vile vile, alisema kabla ya uamuzi huo, aliyekuwa Mwekahazina wa halmashauri hiyo, Edward Mnyoro alikuwa amehamishiwa Shinyanga na kuongeza kuwa watatafuta haki zao wakiwa nje ya kazi.

Mbunge wa Jimbo la Msalala, Kassimu Idd Kassimu, aliwataka madiwani na watumishi kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanafanya kazi kwa uadilifu na kutimiza wajibu wao na thamani ya miradi iendane na fedha zinazotolewa.

"Tuweke uzalendo mbele pande zote mbili madiwani na watumishi tuwatumikie wananchi tusiweke maslahi yetu mbele na kuwapa uhuru madiwani ya kukagua miradi," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Charles Fussi, alisema hayuko tayari kuwavumilia watumishi wazembe wanaoisababishia hasara halmashauri atawapeleka kwa madiwani waamue cha kufanya.

# Stendi ya kisasa Nyamhongolo rasmi kutumika

**Na Pelusy Yohana,** SAUT

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, imetangaza kufunga rasmi stendi ya mabasi ya Buzuruga na kufungua mpya ya Nyamhongolo kwa kiingilio cha Sh. 1,000 kwa abiria anayesafiri.

Kadhalika, imeweka kiwango cha Sh. 1,000 kiingilio kwa mtu yeyote wakiwamo wanaosindikiza ndugu zao ndani ya stendi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, Modesti Joseph, alisema hayo ofisini kwake mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari.

Mkurugenzi huyo aliwataka watumiaji wa stendi ya zamani ya Buzuruga kuanza kuhamia mpya kuanzia leo.

"Kwa sasa tumemaliza miundombinu yote katika stendi hii, ipo tayari kwa matumizi na barabara ya kuingilia iliyokuwa bado sasa ipo tayari kwa matumizi, niwaombe watumiaji wote wa stendi ya zamani ya Buzuruga kuhamia katika stendi hii mpya na kuanza shughuli zao kuanzia Agosti 16, mwaka huu, kwani mpaka sasa kila kitu kipo tayari pamoja na sehemu za kukatia tiketi za mabasi," alisema.

Katika hatua nyingine, mkurugenzi huyo aliwataka watumiaji wa stendi hiyo kuitumia vyema kwa kutunza miundombinu yake ili idumu na kuhudumia watu kwa muda mrefu.

Kuhusu kiingilio katika stendi hiyo mpya, Mkurugenzi Modest alisema kutokana na ubora na mahitaji ya stendi hiyo, kila mtu atakayeingia atalipia kiwango kilichotajwa kwa anayesafiri, wasindikizaji pamoja na magari. Kwa upande wao, baadhi ya wananchi wakiwamo wafanyabiashara katika stendi ya Buzuruga wanaotarajia kuhamia katika stendi hiyo mpya wameiomba serikali kuimarisha ulinzi utakaosaidia kutunza miundombinu.

"Tunatarajia kuhamia sasa katika stendi hiyo mpya ili miundombinu ibaki kuwa salama, tunaomba serikali iweke ulinzi wa kutosha kuilinda pamoja na kutulinda sisi na mali zetu," alisema Philipo Maximilian, dereva wa basi.

"Tumekubaliana kiingilio kilichowekwa, lakini kama ikitokea kuna marekebisho tunahitaji, tutairudia halmashauri itusikilize upya," alisema Kidini Kiheri, mfanyabiashara ndogo ndogo.

Stendi hiyo imegharimu Sh. bilioni 26.6 na inatarajiwa kuanza rasmi kutumika jana ikiwa ni ya kwanza ya kisasa mkoani Mwanza.

Wakati huo huo, stendi nyingine ya kisasa ya Nyegezi inatarajiwa kufunguliwa na kuanza kutumika Oktoba Mosi, 2022.

Stendi ya Nyegezi imegharimu Sh. bilioni 15.8 hadi kukamilika kwake na itakuwa na uwezo wa kuingiza mabasi makubwa 120, na magari madogo 60 kwa wakati mmoja pamoja na kuwapo eneo la biashara ambalo litajumuisha benki, maduka, hoteli na huduma nyingine za kijamii.



Ukurasa 14

**Ndivyo Ruto alivyopenya ngome za Raila Odinga na kumtoa jasho**



Ukurasa 13

Kero hizi zilivyomtibua Kinana Rukwa, Katavi



Ukurasa 12

**Chongolo alipoibua na kumaliza kero zilizokwama miongo kadhaa**

siasa

JUMATANO AGOSTI 17, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

KUANGUKA RAILA

# Pole kwa Odinga licha ya kukaza buti kila uchaguzi

**Na Sabato Kasika**

RAIS wa awamu ya tano wa Kenya, amepatikana baada ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC), kumtangaza Dk. William Ruto kuwa mshindi wa uchaguzi wa Agosti 9, 2022.

Naibu Rais Ruto amemshinda mwanasiasa mkongwe Raila Odinga, mwenye historia ya kuwania urais kila mwaka wa uchaguzi, safari hii ikiwa ni mara ya tano na zote akishindwa.

Nipashe inafuatilia anguko lake, ikizungumza na baadhi ya wachambuzi wa siasa, kuhusu hatima ya mkongwe huyo kama ndiyo mwisho au anaweza kufurukuta tena.


Bob Wangwe, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), anayesema kushindwa kwa Odinga, hakumwondoi kwenye picha kubwa ya mageuzi na demokrasi ya Kenya.

"Odinga ametoa mchango mkubwa. Inawezekana asigombee tena, lakini vyovyote iwavyo ni mwanasiasa aliyetoa mchango katika ujenzi wa demokrasia Kenya ambao si rahisi kufutika. Ni wa kudumu," anasema Wangwe.

Aidha, chama chake kupata wabunge wengi ni dalili kuwa ana nguvu kubwa kwenye siasa za Kenya, na kwamba serikali inayokuja inatakiwa kujikita kuimarisha umoja wa kitaifa ili kuungwa mkono zaidi.

"Chama chake kimepata wabunge 161, huku cha Ruto kikiwa na wabunge 159, pia kuna wabunge 12 ambao hawajatokana na vyama, hivyo ninaamini bunge lao litajikita zaidi katika mambo ya msingi," anasema.

Mchambuzi Gwandumi Mwakatobe, anasema uchaguzi mwingine wa Kenya utafanyika mwaka 2027, na kwamba wakati huo kama Odinga atakuwapo atafikisha miaka 82.



Raila Odinga licha ya kugombea mara tano ameshindwa tena na William Ruto. **PICHA: MAKTABA**

"Kwa sasa ana miaka 77, hivyo kufikia mwaka 2027 umri wake utakuwa umekwenda sana. Ingawa urais si kubeba zege, lakini nadhani atahitaji kupumzika huenda hataweza mchakamchaka," anasema Mwakatobe.

Aidha, anasema ana wasiwasi akifikia umri huo atakuwa ameanza kuwa dhaifu na kwamba inawezekana akashindwa harakati za kisiasa ingawa anaweza kuamua kuendelea kujitosa ulingoni.

"Ninasema hivyo, kwa sababu wapo baadhi ya wanasiasa akiwamo Rais wa sasa wa Zambia, Hakainde Hechilema, hakuchoka hadi mara ya sita akafanikiwa kuingia Ikulu," anakumbusha.

Mchambuzi huyo wa siasa anasema hata Odinga ambaye umri umekwenda, anaweza akaamua kujitosa mwaka 2027 bila kujali umri akafanikiwa au akashindwa tena, kwa kuwa siasa ndivyo zilivyo.

### ANATOA ANGALIZO

Mwakatobe, anafafanua kuwa siasa za Kenya hazina mwelekeo, zinabadilika mara kwa mara, na kwamba Odinga anaweza kujitosa mwaka 2027 na kujikuta anaendelea kupoteza muda badala ya kupumzika.

Anaelezea uwezekano wa kuwapo mabadiliko makubwa katika siasa za Kenya, wakapatikana wanasiasa wengine bora zaidi wenye ushawishi mkubwa kuliko waliopo sasa wakaongoza nchi.

"Ni kwamba, mabadiliko ya Kenya katika siasa hayatabiriki, leo mwanasiasa atakuwa katika chama hiki, kesho kingine au anaungana na adui wake wa kisiasa, hivyo hali ya kisiasa ya baadaye haijulikani," anaeleza.

Anasema katika mazingira hayo, Odinga anaweza kurudi ulingoni akapoteza muda au akafanikiwa akiwa mzee na kumshauri kupisha damu changa.

"Lakini Dk. Ruto bado ana nafasi ya kuwania nafasi hiyo miaka ijayo, kwa sababu umri wake unamruhusu, ikifika 2027 atakuwa na miaka 60, bado atakuwa na nguvu kuliko Odinga," anasema.

Mwakatobe anasema, ingawa Odinga amepata wabunge wengi kuliko Rais Ruto, hawezi kupata vikwazo katika kuongoza nchi, hasa pale atakapoendesha serikali kwa kuzingatia maslahi ya nchi na siyo ya chama.

"Iwapo atazingatia maslahi ya taifa, hata wapinzani watamuunga Ruto mkono, lakini akiegemea chama, anaweza kukutana na vikwazo kuanzia ndani ya chama chake na hata kutoka kwa wabunge wasio na vyama," anasema.

Mwakatobe anaongeza kuwa, siasa za Kenya ni tofauti za Tanzania, na kwamba wakati mwingine hata wabunge wa upinzani wanaweza kuhamia upande wanaouunga mkono kwa maslahi ya taifa.

Anafafanua kuwa, iwapo Rais atakwenda kinyume kwa kuzingatia mambo binafsi, hata wabunge wa chama chake wanaweza kumkimbia na kuhamia kwingine kuweka mikakati ya kutokuwa na imani naye.

### BUNGE LA MVUTANO

Mchambuzi wa siasa, Abdulkarim Atiki, anaamini kwamba Bunge la Kenya litakuwa na mvutano mkali katika kupitisha maazimio na miswada mbalimbali ya serikali, kutokana na idadi ya wabunge inayokaribiana.

"Hilo ndilo ninaloliona katika bunge la Kenya na bahati ni kwamba, wenzetu si watu wa kuburuzwa, hivyo, tutarajie bunge motomoto na lenye kusisimua katika kujadili hoja mbalimbali," anasema Atiki.

Kwenye suala la hatima ya mkongwe wa siasa wa nchi hiyo, Odinga, mchambuzi huyo anasema anaweza kuwa na nafasi nzuri ya kulizungumzia baada ya mahakama kutoa uamuzi.

"Ninasikia amekwenda mahakamani, hivyo tusubiri uamuzi wa mahakama ndipo tuwe katika nafasi nzuri ya kuzungumzia hatima yake, kwani si mara ya kwanza kushindwa katika uchaguzi wa urais," anasema Atiki.

# Chongolo alipoibua na kumaliza kero zilizokwama miongo kadhaa



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akiwa kwenye mkutano na wananchi mkoani Kilimanjaro. **PICHA: MARY GEOFFREY**

**Na Mary Geoffrey**

KATIBU Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, ameanza mwezi Agosti kwa kuwafikia wana Kilimanjaro, huko anaacha furaha miongoni mwa wananchi baada ya kuleta ufumbuzi wa masuala magumu yaliyowatesa kwa muda mrefu.

Akifuatilia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama chake, vilevile kuhimiza ushiriki wa sensa ya watu na makazi, anatatua kero zilizoibuliwa na wakazi wa Moshi Mjini na Same.

Akiambatana na Katibu wa Halmashauri Kuu wa Taifa (NEC), Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Ngemela Lubinga, anafuatilia kero za wananchi, kukagua miradi ya maendeleo kama sekondari, hospitali na ofisi za serikali na chama.

Ziara hiyo inamkutanisha na viongozi na wananchi wa wilaya za Siha, Moshi, Rombo, Mwanga na Same, pia anapokea taarifa za miradi ya maendeleo.

Anaanza kutoa ufumbuzi wa masuala yaliyokuwa yanawatesa wananchi kwa muda mrefu, akianzia wilayani Moshi, anapokea kilio cha kukosa stendi ya mabasi kwa miaka mingi, licha ya serikali kutoa bilioni saba za ujenzi.

Anamtaka Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, kushughulikia ujenzi wa stendi hiyo haraka iwezekanavyo.

Anaziagiza kupanga namna ya kupata fedha za kumalizia mradi huo uliokwama muda mrefu, akisema:"Tuliahidi kuwajengea stendi, ujenzi umeanza fedha zimebakia kiasi imeliziwe ili wananchi waanze kuitumia."

Anaipongeza serikali kwa kutoa bilioni saba kwa ajili ya kazi hiyo kati ya Shilingi bilioni 17 zinazohitajika. Kiwango hicho ni upungufu wa bilioni 27 zilizokuwa zinahitajika awali kabla ya kuondoa majengo ya hoteli yaliyokuwa sehemu ya mradi huo.

> Naomba nimuachie DC, atumie wataalamu kujua fedha zinazohitajika, aniletee ndani ya wiki moja tukishajua gharama nitasaidia kusukuma zipatikane tufanye ukarabati.

"Stendi hii lazima ikamilike, iondoke kuwa hadithi ianze kutumiwa na wananchi wa mkoa huu hususani wa Halmashauri ya Moshi wanufaike na stendi ya kisasa mapema iwezekanavyo," anasema Chongolo.

Anatoa ahadi ya kufuatilia kwa karibu suala hilo na kwamba alishaongea na Bashungwa, anayeahidi kuwa atafuatilia hazina ili fedha zipatikane na kazi ieendelee.

"Tunataka stendi ya Moshi ikamilike, ianze kutumika, tuanze mipango mingine na tuachane na hadithi ya muda mrefu. Nimepewa dhamana ya kumsaidia Rais, naye hawezi kukubali kukutana na maswali ambayo majibu yake ni rahisi na utekelezaji tu," anasisitiza.

Anaongeza kuwa, hawawezi kuendelea kuvumilia kukaa na miradi ya kwenye makaratasi na badala yake anahitaji utekelezaji.

### KUKARABATI SOKO

Chongolo, anakutana na kilio cha wafanyabiashara wa soko la samaki Manyema, wanaotaka kurudishwa sokoni hapo baada ya kuhamishwa na halmashauri kwa madai ya soko kutokidhi vigezo.

Anayasikia malalamiko ya wanawake wafanyabiashara wa samaki, halmashauri iliyowaondoa sokoni hapo mapema mwaka huu na kuhamishiwa soko la Bomambuzi lililoko Pasua.

"Tunaomba, baba tunateseka huu sio umri wa kuteseka kutafuta eneo la kufanyia biashara," Fatma Yusuph anaeleza kwa Katibu Mkuu Chongolo.

Wafanyabiashara wanalalamikia kukosa wateja katika eneo walikohamishiwa pamoja na kuwapo madai ya chuma ulete 'uchawi' wa kupoteza fedha kishirikina.

Katibu Mkuu Chongolo, anamtaka Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, kutoa ufafanuzi wa suala hilo. Kayanda akijibu anasema, halmashauri ilitumia mapato ya ndani kujenga na kukarabati soko la Pasua ili litumike kwa biashara ya samaki.

"Sehemu wanayoisema ilikuwa ya chini ambayo hata kiafya haikuwa salama, kupitia kikao cha baraza la madiwani na vikao mbalimbali Shilingi milioni 250 ziliidhinishwa kukarabati soko la Pasua na kujenga vyoo kwenye maeneo mengine ili wafanyabiashara waishi katika mazingira bora kiafya," anasema.

Hata hivyo, Chongolo anahoji endapo soko hilo likikarabatiwa linaweza kuendelea kutumiwa na wafanyabiashara hao na kutoa siku saba kwa halmashauri kufanya tathimini kufahamu bajeti inayohitajika ili wafanyabiashara warudi sokoni hapo.

Anaahidi, tathimini ikikamilika na kupata gharama inayohitajika atasukuma upatikanaji wa fedha ili ukarabati ufanyike.

"Naomba nimuachie DC, atumie wataalamu kujua fedha zinazohitajika, aniletee ndani ya wiki moja tukishajua gharama nitasaidia kusukuma zipatikane tufanye ukarabati," anasema Chongolo.

### MAJI SAME

Akiwa Same, Chongolo anatoa siku nne kwa Waziri wa Maji, Juma Aweso, kupeleka wataalamu wa kuchimba visima viwili wilayani Same ili kuwapunguzia wananchi adha ya kukosa maji kwa zaidi ya miaka 10, wakati wakisubiri kukamilika mradi mkubwa wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwakani ikiwa ni ahadi ya serikali ya awamu ya nne ambao unagharimu Shilingi bilioni 262, ukilenga kuwafikishia maji wananchi 400,000.

Anamtaka Aweso kutekeleza ahadi yake ya kuwachimbia kisima kimoja wananchi hao, ambayo hajaitekeleza hadi anafika wilayani hapo.

"Sasa badala kisima kimoja njoo uchimbe viwili nami nakupa siku nne uhakikishe hayo magari ya kuchimba yamefika hapa Same kutatua changamoto ya kukosa maji wakati mradi unakamilishwa," anaagiza.

Anaitaka kamati ya maendeleo Wilaya ya Same kusimamia utekelezaji wa mradi huo wa visima ili wananchi wapate maji wakati wakisubiri mradi maji ambao utakamilika miezi sita ijayo.

Akizungumza kwa simu na Chongolo, Waziri Aweso, anaahidi kutekeleza agizo hilo la Katibu Mkuu kwa wakati.

Anaahidi kuwasiliana na wakala wa kuchimba visima waliopo Kijiji cha Msomero, waanze safari ya kuja Same kuanza kazi hiyo.

Kuhusu mradi huo wa maji, anasema wataalamu wapo kazini wanaendelea na kazi na wanatarajia utakamilika miezi sita ijayo na kuukabidhi kwa wananchi.

Januari 19, mwaka jana, serikali ilikabidhi mradi huo wa maji kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) baada ya kusitisha mkataba na makandarasi M.A Kharafi & Sons na kampuni ya Badr East Africa Enterprises, walioondolewa kutokana na kusuasua kwenye kazi hiyo ilianza wakati wa awamu ya nne.

DAWASA, iliahidi hadi kufikia Novemba 30, mwaka jana ungekuwa umekamilika na ungezinduliwa. Mradi huo mkubwa unatarajiwa kuzalisha zaidi ya lita milioni 65 za maji kwa siku.

Mwaka 2010 Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, aliahidi kujengwa mradi huo wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu 2010, lengo likiwa ni kutatua kero ya muda mrefu ya maji katika wilaya za Mwanga na Same mkoani Kilimanjaro na baadhi ya vijiji vya wilaya ya Korogwe Mkoa wa Tanga.

Agizo la Chongolo limeanza kutekelezwa anasema Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Same Mwanga, Christopher Kione, anayewaeleza wanahabari kuwa kazi ya kuchimba visima itakayogharimu Shilingi milioni 172 imeshaanza na kwamba ujenzi wa utakamilika baada ya wiki mbili na kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 42 ya sasa hadi 60.

# Kero hizi zilivyomtibua Kinana Rukwa, Katavi

**Na Beatrice Shayo**

## • Ahoji inakuwaje katazo la mkaa bila mbadala?



Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Abdulrahman Omar Kinana. **PICHA: MTANDAO.**

AKIWA katika ziara ya mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe na Mbeya, Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara), Abdulrahman Kinana, moja ya mambo yanayomchefua ni mwekezaji kuchukua ardhi bila kufidia wamiliki.

Kuchukua ardhi kwa miaka 12 bila kufidia wananchi na kusababisha deni la Shilingi milioni 918, kinaelezwa ni kilio kinachotolewa dhidi ya mwekezaji, aliyechukua viwanja viwili vya ekari 500 kitalu 'A' vilivyoko Kazima Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi.

Wanadai, amezitumia hati za viwanja hivyo kukopa Shilingi milioni 600 kutoka Benki ya KCB, kwa maelezo kuwa anajenga chuo, lakini ameingia mitini, ikielezwa kuwa ilichukuliwa kwa madai ya kujenga Chuo cha Kilimo Katavi (KUA) bila kulipwa fidia.

Anahoji: "Nani aliyekwenda benki kukopa? Nijibuni maana wananchi wanataka haki yao ama muwalipe fedha zao hakuna njia ya mkato, hiyo taasisi ni nani aliyekwenda kuikopea, wawekezaji hao ni kina nani? Hawana kampuni? Wako wapi?"

"Huu ni utapeli, wizi na ufisadi, wananchi wana ardhi yao wamekuja matapeli hii nchi imejaa matapeli wengi. Mtu anasema anataka kuanzisha chuo kikuu kwa mkopo wa Shilingi milioni 600?" Anahoji Kinana.

"Kwa sasa hamjui ni kina nani walichukua hela, kampuni ipi hata hawa watu hamuwajui wako wapi badala yake mnataka kumbebesha mzigo Mkurugenzi wa Halmashauri alipe? Kama KCB hawakudai mkurugenzi unashindwa nini kuwarudishia wananchi hati zao?"

Anaahidi kushughulikia suala hilo ili wananchi warejeshewe hati zao baada ya kuzungushwa miaka 12.

Kinana akiwa mkoani Katavi anawataka viongozi wanaotunga sheria kwa kisingizio cha serikali kwa lengo la kuwaongezea ushuru wananchi kuacha mchezo huo anaosema unawawabebesha mzigo wananchi kushindwa kujikwamua na umaskini.

Anaeleza kuwa, mkulima anayebeba mazao tani moja asidaiwe ushuru na kuwataka wanaofanya mchezo huo kuacha kuwasumbua wananchi.

"Kuna watu wanaoanzisha sheria na kujifanya ni serikali kwa kuwasimamisha wakulima na kuwatoza ushuru wa mazao yaliyo ndani ya tani moja, waache hiyo tabia ushuru ni mpaka uzidi tani moja," anasema Kinana.

Anakumbusha wafanyabiashara wasitozwe kodi kabla ya kuanzisha vitega uchumi, anayasema hayo akiwa Rukwa, akionya kuwa kitendo cha kudaiwa kodi nyingi kabla ya kuanza kazi hakiwafurahishi na kuwataka viongozi wawasaidie.

"Watumishi wa serikali na viongozi kumbukeni sekta binafsi inaanza na wafanyabiashara wadogo ni lazima tuwasaidie tuwapunguzie kero sijui mmenielewa," anauliza Kinana.

> Mtu anataka kufungua biashara anakuja ofisa mazingira hajakaa vizuri OSHA, mara TANROADS na TARURA, Zimamoto, nchi hii tuna mamlaka nyingi za kutoza kodi na si kuendeleza watu maskini.

Anafafanua: "Wenye kuuza mitumba, chakula, karanga tuwapunguzie kero, mtu anataka kufungua biashara ana fedha kidogo labda Sh. 500,000 kabla ya kuanza biashara anaambiwa alete karatasi ya usafi, kibali cha Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA), makisio ya kodi sasa mtaji utakuwa umebaki tena si utakuwa umekwisha."

"Mtu anataka kufungua biashara anakuja ofisa mazingira hajakaa vizuri OSHA, mara TANROADS na TARURA, Zimamoto, nchi hii tuna mamlaka nyingi za kutoza kodi na si kuendeleza watu maskini," anakosoa.

Kinana anashangaa kila anayeingia dukani kwako anakudai, hakuna anayekuja kuuliza shida ili akusaidie biashara ikue badala yake wanaulizia kodi. Anasisitiza kulipa kodi ni sawa lakini wasianze na kodi kabla ya biashara.

### KERO TRAFIKI

Kadhalika, anazungumzia utitiri wa trafiki barabarani kuwa ni kero, anasema hayo wakati akipokea malalamiko mkoani Songwe wananchi wakilalamikia kuwapo kwa trafiki barabarani na kusimamishwa kila mara wakidai askari hao wanawakwamisha.

Wanadai kila kituo wanatoa 2,000 kutokana na makosa madogo ukitoka Mbozi kuelekea Tunduma kuna vituo 15 na askari wamejazana, hivyo hujikuta wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Baada ya kupokea malalamiko hayo ambayo siyo tu kwa mkoa huo bali na kwa maeneo mengine, anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camilius Wambura, kwani ana uhakika IGP ni mwadilifu, hodari na ni mchapa kazi.

Anamshauri IGP, kufanya tathmini ya wingi wa askari wa usalama barabarani hasa mijini, akisema wamekuwa kero.

"Kila baada ya dakika tano gari linasimamishwa zikipita kilometa moja gari zinasimamishwa unaendesha gari yako huwezi kuendesha kwa raha, mabasi hayaendi kwa raha, hakuna raha barabara katikati ya mji, unakwenda hatua moja unasimamishwa mara unaambiwa washa taa sasa niwashe taa ya nini mchana? Nimsihi IGP afanye tathmini ya hali ya trafiki wengi waliopo kwenye miji yetu,"anasema Kinana.

Anafafanua kuwa biashara nyingi zinaharibika, kuchelewa kutokana na kila wakati kuambiwa upaki pembeni anatambua umuhimu wa usalama vile vile wanakerwa na kusimamishwa mara kwa mara.

"Utaambiwa lete leseni, mara lete hiki, mara washa 'waipa' lakini mvua hainyeshi yaani tumekuwa tunawaongezea wananchi kero, mzigo na safari kuwa ndefu kwa sababu ya kusimama simama kila wakati,"anasema Kinana.

Kinana akiwa mkoani Songwe anapokea malalamiko ya wananchi wakidai wamezuiliwa kutumia analosema linamshangaza.

Anawaambia viongozi wanapofanya maamuzi waangalie kipato cha wananchi badala ya kutoa mazuio, akifafanua kuwa wenye kipato cha chini watazamwe kwani sio wote wanamudu kununua gesi, wengi wao wanategemea mkaa na kuni hivyo kuwazuia ni kuwakatili na akawaruhusu kutumia nishati waliyoizoea.

### KUJIPANGIA VIONGOZI

Kupanga safu ya uongozi katika uchaguzi ni taarifa ya malalamiko kutoka kwa wana CCM, mkoani Mbeya, wakidai baadhi ya viongozi wamepanga safu zao katika uchaguzi wa ndani wa CCM, akisema amekerwa na kuwataka wananchi wasiwachague walioandaliwa.

"Ni marufuku kiongozi kujitengenezea safu, anayefanya hivyo hajiamini na hafai kuchaguliwa, msiwachague hawafai nyie ndiyo wapiga kura mnakuja kusema ametengeneza safu," anasisitiza Kinana.

Anawaambia waachane na watoa rushwa, ili apate cheo huyo ni hatari katika jamii, hivyo wasipewe nafasi.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Ndivyo Ruto alivyopenya ngome za Raila Odinga na kumtoa jasho



Rais mteule wa Kenya William Ruto (kushoto) na Naibu Rigathi Gachaua, wakipokea cheti cha ushindi wa uchaguzi kutoka Tume Huru ya Uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WILLIAM Ruto, mgombea wa Chama United Democratic Alliance (UDA), sasa ndiye Rais wa Kenya, baada ya kujizolea kura milioni 7.17 dhidi ya Raila Odinga, mgombea wa Muungano wa Azimio la Umoja la Kenya One, aliyepata kura milioni 6.9.

"Ninatangaza kwamba William Ruto, amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Kenya," ni tangazo la Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC), Wafula Chebukati, linalotolewa jijini Nairobi, likiwaacha Mteule Ruto na mkewe Rachel, wakitabasamu kwa furaha ya ushindi.

Ni safari ya tatu kwa Mwenyekiti Chebukati katika kuongoza uchaguzi mkuu wa Kenya, mara mbili 2017 ambako alisimamia uchaguzi mkuu na marudio ya uchaguzi wa urais. Mwenyekiti wa IEBC ni jina kubwa akiheshimiwa na watu kuwa na imani naye katika mfumo wa uchaguzi.

Chebukati amekuwa na wakati mgumu pamoja na makamishna wengine, waliolengwa na vinara wa Muungano wa NASA wakiongozwa na Raila Odinga na mgombea mwenza Kalonzo Musyoka, Musalia Mudavadi na Moses Wetang'ula ambao walitaka Chebukati ajiuzulu, lakini alikataa.

Zilikuwa enzi za ushindi wa Uhuru Kenyatta na Ruto mwaka 2017, akitakiwa ajiuzulu tume hiyo, ikidaiwa kufanya kinyume na matakwa ya wananchi ambao Raila na timu yake walidai yamekiukwa. Chebukati, alikataa na ameendelea kuongoza IEBC na leo Rais mteule Ruto anamwita shujaa.

> Hatuwezi kuchukua umiliki wa matokeo yatakayotangazwa kwa sababu ya hali isiyoeleweka ya jinsi awamu ya mwisho ilivyoshughulikiwa.



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo, Wafula Chebukati. **PICHA: MTANDAO**

Dk. Ruto, amefaulu mpambano huo ambao una fungamano na misimamo ya kisiasa ambayo imemsaidia kushinda uchaguzi huo ambao sasa ni ushindi wa mseto wa Wakikuyu na Wakalenjin.

Ushindi wa Ruto unatoka kwenye kaunti 10 za Mt Kenya na zile saba North Rift Valley ambazo kwa pamoja zilimpa kura milioni 4.5 na huo ndiyo ushindi wa kishindo kwa mgombea yeyote wa urais kwa kuwa huko ndiko kuna wapigakura.

"Napenda kumshukuru Mungu kwa kutufikisha hapa tulipo. Namshukuru Mungu kwamba leo tumehitimisha uchaguzi huu. Najua kulikuwa na utabiri kwamba sitaingia kwenye kura, lakini kwa sababu kuna Mungu mbinguni tuko hapa," anasema Rais mteule, anayeahidi kuwa hatalipa kisasi dhidi ya wale waliomkwamisha kwa kujaribu kumvurugia azma ya urais.

"Uchaguzi huu unahusu masuala, tofauti na si muundo wa hoja za ukabila umebainisha uchaguzi wetu ni tofauti. Ninajivunia kwamba watu wa Kenya wametuinua tunaotafuta uongozi, siyo kuuza ukabila lakini kuelezea programu na sera zetu," anaongeza, akisema wapiga kura waliinua ilani yake ya kitaifa.

Ili kuingia ikulu na kuwa rais wa tano wa nchi hiyo, Ruto alianza kupanda mbegu kwa mara ya kwanza katika siasa za uchaguzi mwaka wa 1997, akichaguliwa kuwa mbunge wa Eldoret Kaskazini.

Nguzo ya ushindi ni ngome za Mlima Kenya na wapigakura wa Bonde la Ufa ambazo zilikuwa muhimu kwa ushindi wao na Rais Kenyatta mwaka 2013 na 2017, huku pia akizoa kura kwenye ngome za mpinzani wake Raila huko Nyanza, Magharibi na Pwani.

Kaunti 10 za Mlima Kenya na saba za North Rift Valley kwenye Wakikuyu na Wakalenjin ambalo ni kabila lake kwa pamoja zilimpa kura milioni 4.5, ambazo zilitafsiri kuwa asilimia 63 ya kura zake zote, wakati mpinzani wake mkuu, Odinga, akiambulia kura 847,709 kutoka Mlima Kenya na kuanguka zaidi ikionyesha kuwa alikuwa hakubaliki upande wa Kikuyu.

Lakini, kiongozi huyo anakubalika au ilikuwaje ni kuangalia kile kilichotokea kwani hata katika ngome za Odinga, Ruto alipenya kwa wapigakura wa Pwani na upande wa Magharibi na kuzidi kuimarisha ushindi wake.

Mwaka huu mteule Ruto ameona idadi ya kura zake ikipanda Pwani kutoka 287,066 walizopata na Uhuru Kenyatta mwaka 2017 hadi kufikia 324,353 huku kwa Odinga idadi ikushuka katika eneo hilo kutoka kura 801,031 mwaka 2017 hadi 648,834.

Magharibi ngome ya Odinga, Ruto anazoa kura 629,552, karibu mara tatu ya kura 242,000 ambazo Uhuru na Ruto walijipatia mwaka 2017. Mambo hayiishii hapo Ruto alimshinda Odinga katika Kaunti ya Bungoma ya kiongozi wa Ford Kenya, Moses Wetang'ula, akipata kura 255,907 dhidi ya 145,240 za bosi wa Azimio Baba Odinga.

Mnamo 2017, kwenye uchaguzi wa urais kaunti hiyo, ilimpa Odinga kura 284,786 dhidi ya 126,475 za Uhuru na Ruto. Lakini mwaka huu Ruto alikuwa na kura 116,372 dhidi ya 132,404 za Odinga huko Trans Nzoia.

**MAKAMISHNA WAJITENGA**

Ushindi wa Dk. Ruto, hata hivyo, haukung'ara muda wote ulikumbwa na mgawanyiko katika tume ya uchaguzi na mipaka ya majimbo.

Ni baada ya Naibu Mwenyekiti Juliana Cherera, Makamishna Justus Nyang'aya, Irene Masit na Francis Wanderi kujiengua kwenye matokeo hayo, wakisisitiza kuwa mchakato huo haukuwa wa kuaminika na ulifanywa katika "hali isiyoeleweka".

"Hatuwezi kuchukua umiliki wa matokeo yatakayotangazwa kwa sababu ya hali isiyoeleweka ya jinsi awamu ya mwisho ilivyoshughulikiwa," anasema Makamu Mwenyekiti Juliana Cherera. Anapozungumza na wanahabari wakati wa mkutano unaofanyika sambamba Serena Hoteli wakati tume ikitangaza matokeo kwenye ukumbi wa Bomas.

Tume inaundwa na makamishna saba na Mtendaji Mkuu anayeteuliwa miongoni mwao ambaye pia ni katibu wa tume.

Makamishna hao huteuliwa na Rais wa Kenya na kuthibitishwa na Bunge la Kenya. Kila kamishna anahudumu IEBC kwa miaka sita.

Hata hivyo, kwa mujibu wa sheria, kamishna haruhusiwi kuwa mwanachama wa chama cha siasa. Katika maamuzi ni lazima angalau kura nne zinahitajika kwa hatua yoyote rasmi ya tume kufanya maamuzi.



## Wakala kuzalisha chai tani 30,000

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa maendeleo ya wakulima wadogo wa chai Tanzania (TSHTDA) umejipanga kuzalisha tani 30,000 za chai kavu iliyosindikwa ifikapo mwaka 2030 ili kuwainua kiuchumi wakulima wadogo wa zao hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa TSHTDA, Theophord Ndunguru, akizungumza na Nipashe jana, alisema hivi sasa wakulima hao wanazalisha tani 13,000 ambazo hazijitoshelezi, hivyo moja ya mkakati ni kuhakikisha wanaongeza uzalishaji.

"Tumejipanga kuhakikisha wakulima wa zao hilo wanafikia uzalishaji tani 30,000 za chai kavu iliosindikwa, ninaamini tutafikia kiwango hicho kutokana na serikali kutoa mbolea ya ruzuku," alisema.

Ndunguru pia alisema wamejipanga kufanya utafiti wa soko la bei ya chai duniani ili kutatua kero ya wakulima kukosa soko la zao hilo.

Ndunguru alisema kuwa kwa sasa wakulima wanalalama kuuza kwa bei ndogo nchini, jambo linalosababisha kushindwa kumudu gharama za kilimo hicho na hata kupanua kilimo chenyewe.

"TSHTDA kwa kushirikiana na vyama vya ushiriki tumeweka mikakati ya kuhakikisha bei ya chai inapanda ili wakulima waweze kunufaika na kilimo hicho," alisema Ndunguru.

Kuhusu utoaji huduma za ugani, alisema TSHTDA imeingia mkataba na kampuni kwa ajili ya kutoa huduma za ugani wakati wowote kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wamekuwa wakiwafikia wakulima wa zao hilo kupitia maofisa ugani ambao wanatoa elimu ili kufanya kilimo cha kisasa.

Pamoja na hayo, aliwataka wakulima kuchangamkia fursa ya mbolea ya ruzuku iliyotolewa na serikali ili kulima kwa wingi zao hilo.

Ndunguru alisema awali wakulima wadogo wengi walishindwa kumudu kununua mbolea kutokana na bei kubwa, lakini sasa tatizo hilo litatuliwa kutokana na serikali kutoa ruzuku.

Alisema kuanzishwa kwa mfumo wa ruzuku ya mbolea kutasaidia kwa kiasi kikubwa wakulima kuzalisha kwa wingi zao hilo na hivyo kuinuka kiuchumi.

# Tume yajipanga Tanzania yenye uchumi wa kidigitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC) imesema imedhamiria kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kidigitali na kushindana duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Nkundwe Mwasaga, alibainisha dhamira yao hiyo wakati wa kikao cha tathmini ya maendeleo ya mradi wa Tanzania ya Kidigitali kilichofanyika jijini hapo juzi.

"Katika kukuza TEHAMA tunaangalia maeneo manne ambayo ni kukuza wataalamu wa TEHAMA, kukuza kampuni za wabunifu wa TEHAMA, kukuza uchumi wa kidijitali wa kila mkoa na kukuza uchumi wa kidigitali wa Tanzania ili kuongeza ushindani wa nchi duniani.

"Katika kufanya hayo, tunaongeza uwezo vituo vya softcentre (vituo vya kuharakisha na kuongeza uwezo wa wabunifu kuanzisha kampuni) na fablabs (vituo vya kuwawezesha wabunifu kutengeneza bidhaa na mifumo mbalimbali ya kompyuta) ambazo zitakuza ubunifu, pia kukuza kampuni na kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kidigitali utaoiwezesha kushindana duniani," alisema.

Nkundwe alisema watahakikisha uchumi wa kidigitali wa Tanzania unakuwa mkubwa na kuongeza uwezo wa mikoa mbalimbali kupambana katika uchumi wa kidigitali na ndiyo sababu ya kutengeneza vituo hivyo kwenye kanda nne za Mbeya, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam.

"Mpango mpana wa tume ni kuhakikisha vituo hivyo vinakuwapo kila mkoa na kufika kila wilaya Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa kupitia mradi huo, tume ina mambo mawili makubwa inayofanya kwa ajili ya uchumi wa kidigitali.

"Softcentre' zitajengwa Mbeya, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam, vitakuwa ni vituo vya wabunifu ambao watakuwa wanakuja na ubunifu wao na tume itawasaidia kuhakikisha zinakuwa kampuni ndogo zinazoitwa 'startup' kwa ajili ya kukuzwa na kuwa kubwa ili zitoe ajira na kuongeza pato la serikali.

"Hivi vitu tunavyofanya vitatengeneza kazi kwa sababu vijana wakipata kazi ni jambo muhimu sana ambalo litapelekea kuongeza Pato la Taifa kutoka sekta ya TEHAMA," alisema.

Alibainisha kuwa kuanzishwa kwa tume hiyo kunalenga kuhakikisha hayo yanafanikiwa kutokana na kuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera ya TEHAMA nchini.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF), Justina Mashiba, alisema mfuko huo umenufaika na Tanzania ya kidigitali na wanajipanga kuongeza nguvu ya minara 488.

"Tumepanga kuongeza ufanisi wa minara kutoka teknolojia ya 2G, kwenda kwenye teknolojia ya 3G na 4G," alisema.

Alibainisha wanao mradi wa kujenga minara mingine mipya 763 ili lengo la serikali kufikisha mawasiliano kwa wananchi litimie.

"Tuna imani Watanzania walioko vijijini watakuwa na uwezo wa kupata taarifa na kufanya biashara zao kupitia mitandao ya intaneti," alisema.



Meneja Miradi wa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), Edina Chilimo (kulia), akizungumza na washiriki wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kusimamia ruzuku ya fedha za miradi yao, walizopewa na shirika hilo jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge awasilisha hoja kwa waajiri ufanisi sensa

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

ZIKIWA zimesalia siku sita kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi Agosti 23 mwaka huu, Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Dk. Alice Kaijage, amewataka waajiri kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa watumishi ili washiriki ipasavyo.

Dk. Kaijage alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na viongozi wa dini jijini hapo kwa lengo la kuhamasisha kushiriki katika sensa hiyo.

Alisema kuwa takwimu sahihi zitasaidia serikali na wadau kupanga mipango ya maendeleo ya watu wake katika sekta mbalimbali.

Mbunge huyo alisema takwimu sahihi zitakapopatikana zitasaidia kujua idadi ya watu katika maeneo mbalimbali ili kupata huduma za kijamii kwa ubora.

Alipongeza serikali kwa kuendelea na nia ya dhati ya kutoa huduma kwa wananchi kwa kupanga bajeti kwa kuzingatia takwimu sahihi za idadi ya watu wake.

"Niipongeze serikali kwa kujipanga kuendesha sensa ya watu na makazi ambayo itafanyika Agosti 23, mwaka huu, kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu, sura 315, ambayo pia ipo kwenye utekelezaji wa mpango mikakati wa Umoja wa Mataifa wa kufanya sensa ulioanzia 2015-2024," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, aliwataka viongozi wa vyama vya siasa na dini kushirikiana kwa pamoja na serikali kuelimisha jamii na pale inapotokea upotoshaji wawe tayari kukemea.

Dk. Chande alisema lengo la serikali ni kuhakikisha watu wake wanakuwa na maisha bora, hivyo viongozi wa vyama vya siasa na dini waungane kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa sensa.

Katibu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dodoma, Husseni Kuzungu, alisema sensa hiyo isihusishwe na itikadi yoyote ya imani ya kidini wala vyama vya siasa.

Kuzungu alisema sensa ni suala la kiserikali na linatakiwa kuheshimiwa na kushiriki kwa vitendo ili kupata takwimu sahihi kwa maendeleo.

*Imeandaliwa na Magdalena Jackson (SJMC) na Peter Mkwavila





# Kiwanda cha kuchakata matunda chakamilika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa matunda na mboga katika mkoa wa Mbeya, wanatarajiwa kuanza kuongeza thamani ya mazao hayo baada ya kuvuna kutokana na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao hayo kukamilika.

Kiwanda hicho kinajengwa katika uwanja wa ndege wa zamani wa Mbeya na Shirika la HELVETAS ambalo ni miongoni mwa watekelezaji wa programu ya kuboresha mnyororo wa thamani ya kahawa, chai na mazao ya bustani ujulikanao kwa jina la AGRI-CONNECT.

Programu hiyo inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na lengo la ujenzi wa kiwanda hicho ni kupunguza upotevu wa mazao hayo baada ya kuvuna pamoja na kuongeza ubora wa mazao hayo kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Juzi, maofisa mbalimbali wakiwamo wakurugenzi kutoka wizara mbalimbali za kisekta walifanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa kupitia programu hiyo ya AGRI-CONNECT ukiwamo mradi huo wa kiwanda.

Mkurugenzi wa HELVETAS, Daniel Kalimbya, alisema mpaka sasa ujenzi wa jengo la kiwanda hicho umekamilika na kwa sasa wanaendelea na mchakato wa ununuzi wa mashine kwa ajili ya kuchakatia mazao hayo.

Alisema jengo hilo limegawanyika katika maeneo mbalimbali likiwamo eneo la kupokelea matunda na mboga ambapo yatakuwa yanashushwa na magari, eneo la kuoshea, eneo la kupakia na chumba cha baridi cha kuhifadhia mazao hayo ili yakae kwa muda mrefu.

Aidha, alisema ndani ya jengo hilo kuna ofisi mbalimbali kwa ajili ya utawala, vyoo, chumba maalumu cha wazazi kulelea watoto wao pamoja na duka maalum la kuuza bidhaa mbalimbali.

"Hili eneo lina uwezo wa kuhudumia wasindikaji wa matunda na mboga 500, kwa hiyo tunaamini kwamba kiwanda hiki kitakuwa na msaada mkubwa sana kwa wakulima wetu. Mpaka sasa wako wasindikaji ambao wameshaonyesha nia ya kuanza kuchakata," alisema Kalimbya. Baadhi ya wasindikaji wa mazao hayo ambao wanatarajia kuanza kunufaika na kiwanda hicho walisema ujenzi wa kiwanda hicho utawasaidia kuboresha mazao yao na kuyauza kwa bei nzuri ambayo itakuwa inaendana na gharama za uzalishaji.

Mmoja wa wasindikaji hao, Fatma Mbanga, alisema wana kampuni inayozalisha viungo na kwamba kwa muda mrefu walikuwa wanapata shida ya kupata eneo la kuzalishia bidhaa zao.

Alisema kiwanda hicho kitawasaidia kupata eneo ambalo watakuwa wanazalisha bidhaa zao na kuuzia kwa maelezo kuwa katika eneo hilo kuna eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya kuuzia bidhaa hizo.

"Tunaishukuru programu hii ya AGRI-CONNECT kwa kutujengea kiwanda hiki, tunaamini kwamba hili eneo litakuwa msaada mkubwa kwetu maana tutazalisha bidhaa zetu na kuziuza hapahapa," alisema Mbanga.

Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Daines Mtei, aliipongeza HELVETAS kwa kusimamia vizuri mradi huo akidai kuwa ni miongoni mwa miradi iliyotekelezwa vizuri zaidi.

Alisema mradi huo utasaidia kuboresha soko la mazao ya wakulima pamoja na kuwahakikishia wakulima kupata lishe bora tofauti na ilivyokuwa awali.




Mtaalamu wa mazao ya bustani kutoka Shirika la Helvetas, Maxmilian Saku, akizungumza na maofisa mbalimbali kutoka wizara za kisekta waliokagua utekelezaji wa miradi ya programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani wa Agri-Connect, kuhusu ujenzi wa ghala la kuanikia vitunguu la Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Vitunguu cha Igomelo wilayani Mbarali hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wakulima kicheko ruzuku pembejeo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima mkoani Mbeya, wameishukuru serikali kwa kuanzisha mfumo wa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo hasa kwenye mbolea wakidai kuwa ruzuku hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wakulima hao walisema kwa sasa wameanza kujiandikisha kwa ajili ya kuingizwa kwenye mfumo huo wa pembejeo kutokana na maelekezo ambayo wamepewa na serikali.

Mmoja wa wakulima hao, Fabian Mwaluke, alisema mfumo huo utasaidia kushuka kwa bei ya pembejeo hizo tofauti na msimu uliopita ambao walikuwa wananunua kwa bei ya juu.

Alisema kwa sasa wameambiwa kwamba bei ya mbolea msimu uliopita walikuwa wananunua mpaka Sh. 130,000, lakini kwa sasa wameambiwa kwamba bei ya juu zaidi itakuwa Sh. 70,000 baada ya serikali kuingiza ruzuku.

"Msimu uliopita tulishindwa kuhudumia mazao yetu kutokana na bei ya mbolea, wenzetu wengine waliamua kujikita kwenye kilimo cha mazao ambayo hayahitaji sana mbolea," alisema Mwaluke.

Naye Julius Sanga alisema serikali imewasaidia wakulima kupunguza gharama za uzalishaji kwa maelezo kuwa msimu uliopita hakuna zao ambalo lilikuwa na faida kwa wakulima.

Alisema liche ya bei ya mbolea kuwa juu lakini bei ya mazao ilikuwa ya kawaida kiasi kwamba walikuwa hawapati faida nzuri na kwamba wengi waliishia kurejesha fedha zao walizokuwa wamewekeza.

Wakati wa uzinduzi wa mfumo wa ruzuku kwenye mbolea uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Mbeya, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wakulima wote watatakiwa kusajiliwa ili wanufaike na ruzuku hiyo.

Alisema mbolea zote ambazo zitakuwa na ruzuku ya serikali zitakuwa na namba maalumu za utambulisho ambazo zitakuwa tofauti kati ya mfuko mmoja na mwingine ili kuitofautisha na kwamba mtu yeyote akinunua taarifa zitafika serikalini muda huo huo.

# Makarani wa sensa wahimizwa uzalendo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MAKARANI wa Sensa ya Watu na Makazi katika Wilaya ya Chunya, wametakiwa kwenda kuifanya kazi ya kuhesabu watu kwa uzalendo ili kulisaidia taifa kupata takwimu sahihi za watu.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alitoa ushauri huo juzi alipowatembelea makarani hao wanaopata mafunzo katika Shule ya Msingi Kiwanja wilayani hapo na kuwataka kwenda kufuata maadili ya kazi waliyofundishwa.

Alisema serikali imewachagua kwa sababu ina imani kwamba wataisaidia kufanya kazi hiyo na hivyo akawataka kwenda kufanya kazi vizuri ili kuidhihirishia serikali kwamba haikokosea kuwachagua kwenye kazi hiyo.

Alisema siku 19 ambazo wamepatiwa mafunzo maofisa hao ni nyingi na kwamba serikali imewekeza fedha nyingi, hivyo akawataka kuzingatia misingi yote ambayo wamefundishwa na wakufunzi wao.

"Serikali imewaamini ninyi na ndio maana imewaajiri, sasa ni vizuri mkaenda kufanya kazi mkiwa mmetanguliza uzalendo mbele, msipotekeleza majukumu yenu vizuri mtajikuta mnaharibu zoezi," alisema Masache.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema sensa hiyo itaisaidia serikali kwenye upangaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo.

Alisema takwimu zitakazopatikana kupitia sensa hiyo zitasaidia kwenye uboreshaji wa huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo elimu, afya na maji ambazo ni huduma muhimu kwa wananchi.

Mwanginde alisema kwa sasa wanaendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa pamoja na kutoa takwimu sahihi ambazo zitaisaidia serikali kwenye utekelezaji wa miradi ambayo itakuwa inatosheleza mahitaji ya wananchi.

"Sisi tunahitaji takwimu katika wilaya yetu, wilaya yetu ina shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ambazo zitaboreshwa kulingana na idadi yetu, huku kuna wachimbaji, wakulima na wafugaji kwa hiyo tunapotenga maeneo kwa ajili ya shughuli hizi lazima tujue idadi ya watakaokuwa wanatumia," alisema Mwanginde.

Mratibu wa Sensa wa Mkoa wa Mbeya, John Lyakurwa, alisema katika mkoa kutakuwa na zaidi ya makarani 7,000 ambao watakuwa wanafanya kazi katika maeneo mbalimbali.

Lyakurwa alisema kabla ya mafunzo hayo, yalifanyika mafunzo ya walimu wa sensa ambao ndio wanaoendelea kufundisha makarani kwa sasa na kwamba mafunzo hayo yanafanyika kwa nadharia na vitendo.





## CDC yajizatiti kukabili magonjwa ya mlipuko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amesema Shirika la Udhibiti na Usimamizi wa Magonjwa ya Mlipuko (CDC) limeihakikishia sekta ya afya kuwa litaendeleza ushirikiano na nchi za Afrika Mashariki ili kujikinga na maradhi ya mlipuko ikiwamo kipindupindu, UVIKO- 19 na ebola.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano uliowashirikisha mawaziri wa Wizara ya Afya kutoka nchi mbalimbali za Afrika Mashariki katika ukumbi wa Hotel ya Verde, Zanzibar juzi, Waziri Mazrui alisema ushirikiano uliopo kati yao na shirika hilo utasaidia kuyapatia ufumbuzi maradhi hayo.

Alisema mkutano huo utasaidia kujenga mfumo mpya wa kuimarisha ushirikiano kati yao na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika sekta ya afya.

Alisema mkutano huo utawanufaisha na kuwapatia maudhui mazuri watendaji wa sekta ya afya kukabiliana na maradhi hayo pindi yanapotokezea katika nchi zao.

"Azma ya mkutano huu ni kuziwezesha nchi za Afrika Mashariki kujikinga na maradhi ya mlipuko kutoka nchi moja kwenda nyingine," alisema Waziri Mazrui.

Mkurugenzi wa CDC, Dk. Ahmed Ubwe, alisema wapo tayari kufanya kazi kwa ushirikiano kati yao na nchi jirani za Afrika Mashariki ili kuwasaidia kujabiliana na maradhi hayo.

Mkutano huo uliwashirikisha wadau wa afya kutoka nchi za Afika Mashariki na majirani zao. Washiriki wametoka mataifa ya Kenya, Rwanda, Burundi, Somalia na wenyeji Tanzania.

# Migogoro ya ndoa yatajwa chanzo msongo wa mawazo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MIGOGORO ya ndoa na watoto kutelekezwa inasababisha watu kuathirika kisaikolojia na kupata msongo wa mawazo, vijana na wanawake wakiwa ndiyo waathirika wakuu.

Dk. Hafidh Muhammed, mtaalamu wa uchumi, alibainisha hayo jana wakati wa mafunzo kwa vijana, viongozi wa dini na kisiasa ili kuwajengea uwezo wa kukinga na kutatua migogoro katika familia, jamii na Taifa.

Mafunzo hayo yalifanyika kwenye ukumbi wa jengo la Huduma ya Mama na Mtoto Kidongo Chekundu mjini Zanzibar yaliyoandaliwa na taasisi ya vijana (Zanzibar Youth Forum) chini ya ufadhili wa Foundation for Civil Society (FCS).

Dk. Hafidh alisema migogoro inasababisha msongo wa mawazo kwa jamii, akiitolea mfano migogoro ya kifamilia inayosababisha watoto kutelekezwa na hata kuingia kwenye makundi hatari ya kihalifu na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema migogoro wakati mwingine huchangiwa na matatizo ya kifamilia na humpelekea kijana kutenda matendo ambayo hayapaswi kufanywa, pia hali ya uchumi husababisha kuwapo kwa migogoro kutokana na hali ngumu ya maisha na vijana kujiingiza katika vitendo viovu vinavyohatarisha amani ya nchi. Alisema ni lazima kuwajengea uwezo vijana kujitambua na kuacha mambo ambayo yatasababisha migogoro na kuchafua amani iliyoko.

Dk. Hafidh alisema inavyokaribia kipindi cha Uchaguzi Mkuu, Zanzibar hukabiliwa na migogoro ya kisiasa na hufikia hatua wananchi kuwa na uhasama miongoni mwao.

Abdallah Mussa Hija, Meneja wa Miradi wa Jumuiya ya Vijana, alisema wanatekeleza mradi wa kuwafunza vijana, wanasiasa na viongozi wa dini kuhusu mbinu bora za utatuzi wa migogoro ili kupunguza migongano katika jamii.

Alisema mbinu hizo zitasaidia jamii kutambua mbinu bora ya kutatua migogoro inapoibuka, pia kukabiliana nayo pasi na kuleta athari za kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Alisema migogoro katika jamii inatofautiana kutokana na shughuli za watu, akitaja mifano yake inayojumuisha migogoro ya wavuvi, wakulima, wafugaji na ya kisiasa.

Baadhi ya wanufaika wa mafunzo hayo walisema wamejifunza mbinu za utatuzi wa migogoro na kuisaidia jamii kujikinga na migogoro na kuitatua kwa njia ya maelewano bila kutokea machafuko.

"Tumejifunza mambo mengi jinsi ya kutatua migogoro endapo itatokea katika jamii. Jukumu letu ni kuwafundisha wenzetu ambao hawajapata fursa ya kushikiri katika mafunzo haya," alisema Felisiany Issaya Kaimu Mwenyekiti wa Parokia ya Mtakatifu Marco ya Mwera iliyoko nje kidogo mwa Mji wa Zanzibar.

Alisema mbinu mojawapo aliyojifunza katika mafunzo hayo ni jinsi ya kuhamasisha jamii kuwa na utamaduni wa kusamehe ili kuepusha mgogoro usitokee na kuleta machafuko.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, akichuma tango katika maonyesho ya wakulima Nanenane, Kizimbani Zanzibar hivi karibuni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uwekezaji miundombinu ya kisasa kupaisha kilimo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema itaendelea kuweka miundombinu ya kisasa katika sekta ya kilimo ili kukuza sekta hiyo nchini.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alitoa ahadi hiyo juzi alipofunga maonyesho ya kilimo ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya Dole Kizimbani Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni sita kwa ajili ya mradi wa kurejesha urithi wa kijani ambao unalenga kuendeleza uzalishaji wa miche ya miti ya misitu na matunda na upandaji wa miti katika maeneo ya wazi ya mashamba ya serikali na maeneo mengine.

Makamu wa Pili wa Rais alisema fedha hizo pia zitaelekezwa katika utekelezaji wa mradi wa kuendeleza miundombinu ya mifugo maeneo mbalimbali, ununuzi wa mtambo wa uzalishaji gesi ya naitrojeni kwa ajili ya kuhifadhi mbegu za kupandikiza ng'ombe kwa sindano.

Hemed alisema serikali ipo mstari wa mbele katika kujenga na kueneza maendeleo maeneo mbalimbali, akiitolea mfano miradi ya ujenzi wa bababara zitakazosaidia kusafirisha mazao kwa urahisi.

"Ninataka mtambue kwamba serikali yenu ipo mstari wa mbele katika kujenga na kueneza maendeleo mbalimbali vijijini ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya sekta zote za kilimo, barabara za ndani ambazo zitawasaidia wakulima kusafirisha mazao yao kirahisi," alisisitiza.

Hemed alisema mbali na ujenzi wa miundombinu hiyo, serikali imejipanga kuwajengea uwezo wa matumizi ya miundombinu ya umwagiliaji katika kukuza uzalishaji wa mazao ya kilimo, ikitambua asilimia kubwa ya wananchi wanategemea sekta hiyo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeipa kipaumbele sekta ya kilimo ili kuwasaidia wananchi wake kujikimu kimaisha na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora.

Hemed alipongeza uongozi wa Wizara Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kuendelea kuandaa maonyesho hayo na kueleza kuwa ni wajibu kwao kuendeleza ushirikiano na juhudi ili sekta ya kilimo itoe matokeo yanayotarajiwa katika jamii.

Waziri wa Kilimo, Shamata Shaame Khamis, alisema wizara imejipanga kuhakikisha wanalizungushia uzio eneo lote ambalo linafanyiwa maonyesho hayo ili kulitunza na kuimarisha ulinzi ikiwa na maelekezo kutoka kwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyoyatoa alipokuwa akiyafungua maonyesho hayo.

Waziri huyo alisema atahakikisha eneo la maonyesho linatoa huduma bora kwa kila mtu anayefika katika maonyesho hayo ili kuleta ufanisi mzuri kwa wananchi huku akiomba uungwaji mkono wa wadau katika sekta ya kilimo na ufugaji.

Alisema wizara yake imejipanga kuleta wawekezaji kuwekeza katika sekta ya ufugaji ili kuhakikisha Zanzibar inajitegemea kwa kila kitu, hasa kwa chakula.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Seif Shaaban Mwinyi, alisema katika maonyesho hayo yaliyoanza Agosti 6 mwaka huu, wananchi wamepata fursa ya kujifunza kilimo cha kisasa na ufugaji wenye tija na lengo kuu la maonyesho hayo ni kuwasaidia wananchi kupata elimu na kulima kilimo cha kisasa na chenye tija ili kuondokana na utegemezi wa chakula.

Shaaban alisema maonyesho ya mwaka huu yamevutia washiriki wengi, wakiongezeka na kufikia 225 kupitia sekta mbalimbali za kiserikali na binafsi wakiwamo wajasiriamali kulinganisha na miaka iliyopita, akisisitiza wizara imejipanga kutumia zaidi ya Sh. milioni 600 kwenye maonyesho hayo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

**FATUMA AZIZI KALOYA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI **(NISSAN-KLUGER)** yenye namba za usajili **T 454 DKF** Chasis Namba: **ACU200029387** Engine Namba: **2AZ0634720** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **DSM/PHQ/RB/196796/2022**

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

**ALEX MKAMA MFALIGUNDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **TOYOTA** Corona yenye namba za usajili **T 996 AMG.** Chassis no. **ST2100002723,** Engine no. **3S2029770.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/315398/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BAGAMOYO**
**Kituo cha KEREGE Mkoa PWANI**
**Shauri la madai/Ndoa Na 37/2022**
**Jina la mdai EMMANUEL DIONIS NJAU**
**Jina la mdaiwa AGNESS EMMANUEL JUMBE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa AGNESS EMMANUEL JUMBE**
**BAGAMOYO-UDINDIVU**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)**

**KUJIBU MADAI –NDOA/TALAKA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 29 mwezi 8 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 15 mwezi 8 mwaka 2022**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KEREGE BAGAMOYO

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**MATRIMONIALCAUSE NO.149 OF 2022**
**JULIAN S. MOSHA ......... PETITIONER**
**VERSUS**
**JOHNSON F. BIHONDWA .........RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 18 day of August ,2022 at 8:30 am Before HON. SWAI SRM
YOUR required to appear in this court without failure and you mast produce to that day all the documents upon which you intended to reply in support of your case.
**Given under my hand and seal of the court this 13 day of July, 2022**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

**MARIA DAVID SANGUSANGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **TOYOTA TOWNACE** yenye namba za usajili **T 684 DPP.** Chassis no. **JT711SR4000210270,** Engine no. **3FE10270.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/317558/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya mwanzo ya THEMI**
**Wilaya ya ARUSHA**
**MADAI YA TALAKA YA 42/2022**
**MDAI MELCKIORY JOACHIM MASSAE**
**Amdai**
**Mdaiwa WINNE. T. MOSHA**

**Kwa WINNIE .T.MOSHA**
**DAR- ES -SALAAM,**
**0768421196.**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai).**

**UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMA KUJA KUJIBU MADAI YA TALAKA.**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binaffsi katika Mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 19/09/2022 saa 3:00 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hili, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohudus shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Singatia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 15/8/2022

..............................
**Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OLEN MANASE SANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA COASTER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.738 ANZ** RANGI YA MULTICOLOUR. CHASSIS NAMBA **HZ B500001640.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/324611/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NAMBA 78 YA MWAKA 2021**
**MUSULICHE LEBELWA.........MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **NATIONAL INSURANCE CORPORATION**
- **BAM INSURANCE AGENCY**
- **ALEXANDER A. MALLAY**
- **IDDI OMARI**

**WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**

- **BAM INSURANCE AGENCY,**
  **DAR ES SALAAM**

**ALEXANDER A. MALLYA**
**DAR ES SALAAM**

- **IDD OMARI**
  **DAR ES SALAAM,**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya jinai zinazopatikana katika mahakama hii, unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambae anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 07/09/2022 saa tatu (3:00) asubuhi mbele yam he. Jaji E. E. Kakolaki, kujibu madai hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.
ANGALIA: Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini , basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
**HATI hii imetolewa kwa MKONO WANGU na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 29 mwezi 07 2022**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOVENARY KATEBARIRWE JASSON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4802-0054** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **CHITWE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018.** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: IGU/RB/908/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JUSTA J. JAMES** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index **NO. S0205-0085** kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia **KIBOSHO GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2014.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/269702/2022**

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

**NDUGU HAJI HARUNA SALEHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T346CGY aina ya TOYOTA VITZ** yenye Eng. **No.1SZ0933628** na Chasis No. **103306486** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/323831/2022**


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Machinga warejea kinyemela maeneo yasiyo rasmi

**Victoria Mgodomi na Owen Bariki,**

TUDARCo

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu Machinga mkoani Dar es Salaam, wameendelea kufanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi licha ya agizo la serikali kuwataka kuhama kwenda maeneo rasmi waliyopangiwa.

Juzi, Nipashe ilitembelea baadhi ya maeneo na kukuta wafanyabiashara hao wakiuza bidhaa zao pembezoni mwa barabara, maeneo ya watembea kwa miguu, maegesho ya magari, nje ya maduka na masoko hali inayoleta usumbufu mkubwa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao anayeuza nguo za mtumba na kupanga pembezoni mwa barabara eneo la Mchikichini, Fadhius Selemani, alisema analazimika kufanya biashara eneo hilo kwasababu alikohamishiwa hakuna wateja.

"Kwanza serikali imetuondoa bila kutuambia sababu, kwani hapa kuna shida gani ya kuuza, huko wanakotaka tukauzie (Machinga Complex) hakuna wateja, unakaa siku nzima hata Sh. 100 hupati," alisema.

Naye Charles Bakari anayeuza bidhaa za urembo njia ya watembea kwa miguu barabara ya Mwenge - CocaCola, alisema: "Sioni tatizo kufanyabiashara eneo hili kwa kuwa ninapata wateja, kuniondoa hapa ni uonevu kwa kuwa ninapata wateja."

"Nina mke na watoto wawili ambao wanategemea biashara hii wale na wapate huduma za msingi, sasa nikisema niende huko ambapo serikali inataka ilhali hakuna wateja familia yangu nitaihudumiaje? Serikali inapaswa iliangalie hili," alisema.

Kwa upande wake, Justine Matias, mfanyabiashara wa nguo alisema kinachowafanya waendelee kukaa eneo la Mwenge, ni mazoea kati yao na wateja, akiondoka eneo hilo atawapoteza.

"Sio kwamba sitaki kuhama katika eneo hili napenda kuhama hata leo, kwa sababu hata sisi tunaathirika na vumbi la barabarani na pia tunagongwa na pikipiki na magari. Lakini sasa wateja wetu wameshazoea wakija wanatukuta hapa, inabidi tu nikomae," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya Soko la Mchikichini, Ramadhan Gwamila, alisema suala hilo ni kero kwa sababu wafanyabiashara waliokaa maeneo rasmi wanashindwa kufanya biashara kutokana na wateja wote kuishia nje kwa Machinga wasio katika maeneo rasmi.

Alisema, serikali iliamua kuwaondoa ili kuweka mpangilio mzuri wa mji, lakini mazoea ndiyo chanzo cha wao kurudi katika maeneo hayo na kuiomba serikali kuongeza nguvu ili kuwadhibiti.

# Magari kupita daraja jipya Wami mwezi ujao

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema serikali inatarajia kuanza kuruhusu magari kupita katika daraja jipya la Wami lililoko mkoani Pwani Septemba, mwaka huu.

Alitoa taarifa hiyo jana wakati akikagua maendeleo ya daraja hilo pamoja na mambo mengine alimtaka mkandarasi kukamilisha kazi zilizobakia katika daraja hilo ili kurahisisha matumizi salama ya watumiaji.



Mbarawa alisema: "Hadi sasa kazi zinaendelea vizuri, ni matumaini yangu hadi kufikia Septemba 20, mwaka huu mtakuwa mmeshakamilisha kazi zilizobaki ili mimi niweze kuruhusu magari kupita."

Alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 86, utekelezaji wake unajumuisha ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 513.5 pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 3.8. Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya kimkakati na kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji nchini.

Akitoa taarifa ya mradi, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Pwani, Mhandisi Heririsper Mollel, alieleza kuwa mkandarasi amekamilisha ujenzi wa sehemu ya chini ya daraja hilo kwa asilimia 100 na sehemu ya juu amekamilisha tabaka la juu la lami mita 256 kati ya mita 513.5 ambayo ni sawa na asilimia 50 ya urefu wa daraja.

Mhandisi Mollel alisema kuwa kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa makalvati makubwa matatu na madogo saba na uwekaji wa mabomba 188 ya maji kati ya 206 ambayo ni sawa na asilimia 91.

Kuhusu ujenzi wa barabara unganishi, Mhandisi Mollel alisema kuwa kazi hadi sasa kilomita 3.4 za ujenzi wa tabaka la lami la chini zimekamilika.

Ujenzi wa daraja jipya la Wami unagharimu zaidi ya Sh. bilioni 75 ambazo zimetolewa na serikali, unatekelezwa na Mkandarasi Power Construction Corporation kwa muda wa miezi 48.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kulia), akipitia mpango kazi wa ujenzi wa daraja jipya la Wami lenye urefu wa mita 513.5 na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 3.8, wilayani Chalinze, mkoani Pwani jana, linalotarajia kuanza kutumika mwezi ujao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi madai kutumia jina la Waziri Mkuu kujipatia fedha yaahirishwa

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kutumia jina la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kujipatia Dola za Marekani 10,000 inayowakabili mjasiriamali Bahati Malila na mchapishaji Godfrey Mtonyi (30), imeshindwa kusikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya upande wa Jamhuri kutokuwa na shahidi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate kuwa kesi hiyo ililetwa kwa ajili ya kusikilizwa lakini hawana shahidi.

Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba Mosi, mwaka huu, saa 3:00 asubuhi.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka sita likiwamo la kuongoza genge la uhalifu. Inadaiwa kati ya Januari 3 hadi 31, 2020 jijini Dar es Salaam, kwa pamoja waliongoza genge la uhalifu au kufanya mchoro wa uhalifu.

Katika shtaka la pili na tatu, inadaiwa siku hiyo na eneo la Msasani, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, washtakiwa hao walighushi cheti cha mchango kikionyesha ni cheti halali kilichotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Katika shtaka la nne, washtakiwa wanadaiwa kutoa nyaraka za uongo ambazo inadaiwa Januari 14, 2020 eneo la Msasani, walitoa nyaraka za uongo kwa Guanhn Su Biaolin Tang, ikionesha ni cheti halali kilichotolewa na Waziri Mkuu Majaliwa.

Shitaka la tano, inadaiwa siku hiyo na eneo hilo hilo, washtakiwa waliwasilisha cheti cha uongo kwa mtu huyo wakiwa na lengo la kupata msaada.

Katika shtaka la sita, washtakiwa hao walijipatia Dola za Marekani 10,000, sawa na Sh. milioni 22.9 kwa kudai fedha hizo ni msaada ambao unapelekwa kwa Waziri Mkuu.

# LUSAJO AIPONGEZA TPLB KURUHUSU WAGENI 12 KUCHEZA MECHI MOJA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Namungo FC, Reliants Lusajo, ameipongeza Bodi ya Ligi nchini (TPLB) kwa kupitisha kanuni mpya inayoruhusu kusajiliwa kwa wachezaji 12 wa kigeni na wote kuruhusiwa kucheza katika mchezo mmoja, kwa kueleza kwamba kutaongeza chachu kwa wazawa kujituma zaidi ili kupambania namba katika vikosi vya timu zao.

**Kabla ya maboresho hayo, klabu zilikuwa zinaruhusiwa kusajili wachezaji wa kigeni wasiozidi 12, lakini ziliruhusiwa kuchezesha wachezaji wanane tu katika mchezo mmoja.**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari ya Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, wiki iliyopita kabla ya mchezo wa Ngao ya Jamii Jumamosi kati Yanga na Simba, ilieleza kuwa Kikao cha Kamati ya Utendaji cha Shirikisho la Soka nchini (TFF), kilichoketi Agosti 9, mwaka huu jijini Arusha, kilipitia maboresho ya Kanuni za Ligi Kuu, na wadau wengi walipendekezo kipengele hicho kiboreshwe.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya juzi timu yao kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Lusajo alisema kipengele hicho kilikuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wadau wa soka ambao walikuwa wanahoji ni kwa nini klabu ziruhusiwe kusajili wachezaji 12, lakini ni wanane tu waruhusiwe kwa mechi moja.

Alisema kanuni hiyo ya wachezaji 12 kucheza katika mchezo mmoja, italeta chachu kwa wachezaji wazawa kupambana ili kupata nafasi ya kucheza na kusaidia timu zao.

Lusajo alisema ujio wa kanuni hiyo una mambo mawili ikiwamo faida kwa timu kupata nafasi ya kutumia wachezaji hao na kuweza kupata matokeo mazuri lakini kuleta changamoto kwa wazawa kutaka kuonyesha uwezo wao.

"Pia kuna hasara kwa taifa kwa sababu inafanya wachezaji wengi wa kigeni kupata nafasi huku wazawa wakishindwa kupata nafasi ya kucheza katika kikosi jambo hili linaweza kuiua taratibu timu yetu ya taifa," alisema Lusajo.

Alisema mamlaka inapaswa kulitazama hilo kwa kuipitia kanuni hiyo ili kujenga timu ya taifa bora kwa kuwezesha wazawa kuendelea kupata nafasi ya kucheza.

"Kwa kuwa hiyo kanuni ndio inaanza msimu huu, wachezaji wazawa tunatakiwa kupambana hii kwetu ni changamoto ambayo tunatakiwa kucheza nayo kwa kujituma zaidi ili kupata namba katika kikosi cha kwanza," alisema Lusajo ambaye msimu uliopita alimaliza na mabao 10 kwenye Ligi Kuu Bara.

**AMBAA...**



Mchezaji wa All Stars Veteran ya Mbezi Tangi Bovu, Rafiki Ntoke, akiambaa na mpira katika mechi ya kirafiki dhidi ya Ukonga Veteran iliyopigwa viwanja vya Jakaya Kikwete, Kidongo Chekundu jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Julio: Ligi hii Simba, Yanga vipigo vipo

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amefunguka kuwa kwa jinsi alivyoziona timu za Ligi Kuu, msimu huu wa 2022/23, utakuwa na ushindani mkubwa na timu yoyote ikijichanganya, iwe Simba ama Yanga, itachezea kichapo.

Namungo ilianza msimu juzi kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar katika mchezo wake wa kwanza uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Julio alisema ligi ya msimu huu itakuwa ngumu kuliko ya msimu uliopita kutokana na usajili uliofanywa na timu zote na kwamba timu yoyote inaweza kuchezea kipigo na si ugenini tu bali hata nyumbani.

"Timu zimejitahidi kufanya usajili wa kutosha, hakuna timu nyonge katika ligi ya safari hii, hii ni kutokana na Azam kuweka donge nono kwenye ligi, hivyo timu zote zipo vizuri na zimejiandaa vema.

"Hakuna timu ya kuibeza, yoyote itakayojichanganya itachezea kichapo si nyumbani wala ugenini na si Simba wala Yanga, hakuna ambayo inaweza kujihakikishia ushindi," alisema Julio.

Kuhusu matarajio ya timu yake, alisema amejipanga kuhakikisha anatwaa ubingwa wa ligi ama kushika nafasi nne za juu.

Ligi hiyo itaendelea kwa mechi nne kuchezwa ambapo Simba itaikaribisha Geita Gold FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku Azam FC ikiwa nyumbani kuialika Kagera Sugar, Dodoma Jiji FC ikiwa mwenyeji wa Mbeya City katika Dimba la Liti mkoani Singida wakati Coastal Union ikiikaribisha KMC FC.



# Uwanja wa bao la kwanza Ligi Kuu wafungiwa

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Ruvu Shooting, Ally Bilal, ameweka rekodi ya kufunga bao la kwanza la msimu wa Ligi Kuu 2022/23 juzi, timu yake ikicheza dhidi ya wenyeji Ihefu FC kwenye Uwanja wa Highland Estate, Mbarali Mbeya, huku uwanja huo ukifungiwa baada ya mechi hiyo.

Bilal aliyesajiliwa msimu huu na Ruvu Shooting akitokea JKT Tanzania, amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao msimu huu dakika ya 18 ya mchezo ambalo lilidumu hadi kipenga cha mwisho, timu yake ikiondoka na ushindi wa bao 1-0 ugenini.

Kwa bao hilo, Bilal amevunja rekodi ya mchezaji William Edgar wa Mbeya Kwanza, ambaye kwa sasa amejiunga na Kagera Sugar, aliyefunga bao la ufunguzi msimu uliopita dhidi ya Mtibwa Sugar dakika ya 49, ambalo pia liliipa ushindi wa 1-0 timu hiyo kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi Pwani, Septemba 27, mwaka jana wakati Mtibwa ikiutumia kama uwanja wake wa nyumbani.

Mechi ya kwanza msimu uliopita na msimu huu zimekuwa na mfanano, kwani pamoja na wachezaji hao kufunga mabao ya ufunguzi ambayo yamekuwa hayarudishwi au kuongezwa, timu zilizocheza ugenini ndizo zilizoshinda.

Baada ya mechi hiyo, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kupitia kamati yake ya leseni za klabu, ikaufunga uwanja huo kwa kutokidhi vigezo.

Uwanja huo ambao awali ulipitishwa, ulifungiwa ghafla baada ya mechi hiyo kurushwa laivu na eneo la kuchezea likionekana lina mapungufu.

Katika taarifa yake jana, TFF kupitia kamati hiyo ilieleza kuwa utelekezaji huo unaanza mara moja na klabu ya Ihefu inatakiwa kuchagua uwanja mwingine miongoni kwa viwanja vilivyopitishwa na kamati husika.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UTD YAMTAKA AUBAMEYANG

KLABU ya Manchester United ipo tayari kupambana na Chelsea kwa ajili ya kumchukua mshambuliaji Mgabon, kutoka Barcelona mwenye umri wa miaka 33, Pierre-Emerick Aubameyang. ***(Sun)***

### VARDY NAYE AWINDWA

MANCHESTER United wanaangalia uwezekano wa kumsajili mchezaji wa Leicester City, Jamie Vardy mwenye umri wa miaka 35, lakini 'Mbweha' hao wanasemekana kusitasita kumruhusu mshambuliaji huyo. ***(Athletic via Daily Star)***

### RONALDO KUONDOKA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amejiandaa kumruhusu mshambuliaji wake, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 kuondoka katika klabu hiyo. ***(Times)***

### GORDON AWINDWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imejipanga kuboresha ofa yao ya pauni milioni 45 kwa ajili ya winga wa Everton, Anthony Gordon, baada ya kuona dau la kwanza la pauni milioni 45 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 limekataliwa. ***(Times)***

### SEMENYO AGOMBEWA

KLABU ya Crystal Palace inajiandaa kulipa pauni milioni 12 kwa ajili ya mshambuliaji Mghana Antoine Semenyo, huku kukiwa na nia ya mchezaji huyo kutoka Bournemouth na Everton. ***(Mail)***

### NUNES AWINDWA

KIUNGO wa kati wa Sporting na mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Matheus Nunes amejiunga na Wolves kwa ada iliyoweka rekodi ya malipo ya juu ya euro milioni 45. Liverpool na West Ham zimekuwa zikihusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Record)***

### CASADEI AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA pia wanakaribia kushinda kinyang'anyiro cha kumchukua kiungo wa kati wa Inter Milan mwenye umri wa miaka 19, Cesare Casadei. ***(Guardian)***

### PEDRO BADO NEWCASTLE

OFA ya Newcastle ya pauni milioni 20 kwa ajili ya mshambuliaji wa Watford, Joao Pedro mwenye umri wa miaka 20, imekataliwa. ***(Sky Sports)***

### PALMIERI NA WEST HAM

KLABU ya West Ham imewasiliana na Chelsea kwa ajili ya kusajili mlinzi wa kushoto mwenye umri wa miaka 28, Emerson Palmieri. ***(Fabrizio Romano)***

### KEHRER KUNG'OLEWA PSG

WEST Ham pia wana nia na mlinzi wa Paris St-Germain, Thilo Kehrer mwenye umri wa miaka 25, huku wakijaribu kupambana kuimarisha safu yao ya ulinzi. ***(Sun)***

### DE JONG BASI TENA UTD

OFA ya Manchester United ya kumnunua kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Barcelona, kwa sasa imepitwa na wakati. ***(Kick-off of De Telegraaf via Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP AKERWA KADI NYEKUNDU YA NUNEZ

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema atazungumza na Darwin Nunez baada ya mshambuliaji huyo aliyenunuliwa kwa fedha ndefu kupewa kadi nyekundu wakati Liverpool ikitoka sare ya bao 1-1 na Crystal Palace, Jumatatu usiku.

**Mchezaji huyo wa Uruguay tayari alikuwa na mechi ya kwanza ya kukatisha tamaa baada ya kupiga mashuti matano ambayo hayakulenga goli, kabla ya kuonyeshwa kadi nyekundu kwa kumpiga kichwa Joachim Andersen ambaye alimsukuma.**

Liverpool walitawala mchezo huo pale Anfield licha ya kucheza zaidi ya theluthi moja ya mchezo wakiwa na wachezaji 10, lakini walikatishwa tamaa na timu shupavu ya Palace ambao wangeweza hata kuchukua pointi zote tatu baada ya Wilfried Zaha kukosa nafasi ya kufunga dakika ya mwisho.

> ●●● Anajua hilo yeye mwenyewe kwamba alifanya makosa na nitazungumza naye...

Zaha aliwapatia wageni bao la kuongoza katika kipindi cha kwanza baada ya kukimbilia mpira uliopigwa na Eberechi Eze na akamfunga Alisson kwenye kona ya mbali ya kulia. Luis Diaz, aliisawazishia Liverpool muda mfupi baada ya Nunez kutolewa, akiwapiga chenga wachezaji kadhaa upande wa kushoto kabla ya kupiga shuti kwenye kona ileile ya wavu aliyopata Zaha mapema.

Akizungumza na Sky Sports, baada ya mchezo huo kumalizika, Klopp alisema, Nunez alijua alifanya makosa, lakini akaongeza kwamba atalazimika kuzoea hali ya ulinzi kwenye Ligi Kuu ya England.

"Anajua hilo yeye mwenyewe (kwamba alifanya makosa) na nitazungumza naye," alisema boss wa Wekundu hao.

"Haina maana sana kwamba ninazungumza juu yake hadharani. Sio maoni unayotaka kuona."

Klopp alifurahishwa zaidi na mchango wa mshambuliaji wake mwingine wa Amerika Kusini, Diaz, ambaye bao lake liliifanya Anfield kuwa hai huku wenyeji wakijaribu kulazimisha bao la ushindi, wakati Mohamed Salah na mchezaji wa akiba, Fabio Carvalho wote wakikosa nafasi ya kufunga dakika za mwisho.

"Luis alicheza mchezo wa hali ya juu, hasa baada ya bao, alicheza kama wachezaji watatu au wanne," aliongeza Klopp.

"Bao la ajabu na bila shaka, tulihitaji hilo, kisha tukapata nafasi mbili nzuri kutoka pembeni (ya eneo la hatari), moja na Fabio, moja na Mo, lakini mwisho hatukupata ushindi."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,023,1

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 18 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/08/22 | 19:00 | Rakow Czestochowa vs Slavia Prague | 2.73 | 3.24 | 2.53 |
| 02. 18/08/22 | 19:30 | El Gouna vs Ghazl EL Mahallah | 2.50 | 2.86 | 3.07 |
| 03. 18/08/22 | 19:30 | Al Masry Club vs Ismaily SC | 2.39 | 2.86 | 3.26 |
| 04. 18/08/22 | 20:00 | Pyunik Yerevan vs Sheriff Tiraspol | 2.83 | 3.13 | 2.52 |
| 05. 18/08/22 | 20:00 | Apollon Limassol vs Olympiakos | 3.37 | 3.22 | 2.16 |
| 06. 18/08/22 | 20:00 | CSKA Sofia vs FC Basel | 3.04 | 3.24 | 2.32 |
| 07. 18/08/22 | 20:00 | BSC Young Boys vs Anderlecht | 2.16 | 3.48 | 3.13 |
| 08. 18/08/22 | 20:00 | Maccabi Tel Aviv vs Nice | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 09. 18/08/22 | 19:00 | HJK Helsinki vs Silkeborg | 2.87 | 3.22 | 2.43 |
| 10. 18/08/22 | 21:00 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.63 | 3.23 | 2.63 |
| 11. 18/08/22 | 21:00 | Zrinjski Mostar vs Slovan Bratislava | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 12. 18/08/22 | 21:15 | Maribor vs CFR Cluj | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 13. 18/08/22 | 22:00 | Austria Vienna vs Fenerbahce | 2.78 | 3.29 | 2.46 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TUCHEL, CONTE KIKAANGONI

**LONDON,** England

CHAMA cha Soka cha England, kimethibitisha kuwa, Thomas Tuchel na Antonio Conte wameshtakiwa kwa utovu wa nidhamu katika mchezo wao wa sare ya mabao 2-2 kati ya Chelsea na Tottenham Hotspur uliochezwa Jumapili.

Wawili hao walishambuliana wakati wa mchuano huo mkali na ilibidi watenganishwe wakati wa kuagana kwa kupeana mkono kuligeuka kuwa mechi ya kurushiana maneno.

Taarifa ya FA ilisema: "Thomas Tuchel na Antonio Conte wote wameshtakiwa kwa kukiuka Kanuni ya E3 ya FA, baada ya mechi ya Ligi Kuu England kati ya Chelsea FC na Tottenham Hotspur FC Jumapili ya Agosti 14, mwaka huu.

"Inadaiwa kuwa tabia ya wasimamizi wote wawili haikuwa sawa baada ya kumalizika kwa mechi.

"Thomas Tuchel na Antonio Conte wana hadi Alhamisi ya Agosti 18, mwaka huu kutoa majibu yao husika."

Hasira zilipamba moto hapo awali Pierre-Emile Hojbjerg alipofanya matokeo kuwa bao 1-1, kabla ya Reece James kuwaweka tena mbele 'The Blues' hao.

Bao la kusawazisha la Harry Kane la dakika ya 96 lilishuhudia timu hizo zikigawana pointi moja moja kabla ya Tuchel na Conte kutaka kuzichapa baada ya kipenga cha mwisho kulia.

Wawili hao walionekana kudharau tukio hilo katika maoni yao baada ya mechi, ingawa baadaye Conte aliandika kwenye akaunti yake ya Instagram: "Bahati nzuri sikuona chochote kibaya."




# Allegri hana wasiwasi na jeraha la Di Maria

**TURIN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Juventus, Massimiliano Allegri, amesisitiza kuwa "sina wasiwasi" kuhusu Angel Di Maria baada ya Muargentina huyo kuondoka uwanjani akichechemea kwenye mchezo dhidi ya Sassuolo.

Di Maria alifunga bao lake la kwanza na kutoa pasi ya bao kwa Dusan Vlahovic katika ushindi wa mabao 3-0, ambapo mshambuliaji huyo pia alifunga kwa penalti.

Baada ya kuanza kwa taratibu, ilikuwa rahisi sana kwa Juventus baada ya bao la kwanza la Di Maria, lakini wasiwasi ulizuka kutokana na mchezaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain kutoka nje kipindi cha pili akiwa ameumia.

Juventus pia, ilishuhudia Denis Zakaria akipata jeraha wakati wa mechi, lakini Allegri alisisitiza kwamba hakuwa na wasiwasi.

"Sina wasiwasi. Tutaona vipimo vitakavyosema kesho (leo)," alisema Allegri akiiambia DAZN.

"Kwa bahati mbaya, mambo haya yanatokea kwenye soka. Alikuwa na tatizo hili nyongeza wiki moja iliyopi pia, labda ningemtoa tuli okuwa mbele kwa mabao 3-

"Zakaria alikuwa na kig gumizi, hakuna zaidi. Jamb muhimu ni kwamba tulishi da mchezo tuliotaka kus inda, ambao haukuwa rahis

Juventus huenda wak ongeza wachezaji wengi kabla ya kufungwa kwa di sha la uhamisho Septemb Mosi, mwaka huu huku mch zaji mwenzake wa zamani Di Maria kule PSG, Leand Paredes akipigiwa upatu k hamia Turin.

## HABARI MICHEZO

# 154,178/-

## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/08/22 | 17:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 02. 20/08/22 | 17:00 | Fulham vs Brentford | 2.39 | 3.28 | 2.93 |
| 03. 20/08/22 | 17:00 | Preston vs Watford | 2.89 | 3.14 | 2.49 |
| 04. 20/08/22 | 17:00 | Birmingham vs Wigan | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 05. 20/08/22 | 17:00 | Swansea vs Luton Town | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 06. 20/08/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.85 | 3.39 | 2.39 |
| 07. 20/08/22 | 17:00 | Forest Green vs Plymouth | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 20/08/22 | 17:00 | Burton vs Port Vale | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 09. 20/08/22 | 17:00 | Doncaster vs Salford City | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 10. 20/08/22 | 17:00 | Colchester vs Leyton Orient | 2.98 | 3.33 | 2.33 |
| 11. 20/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs AFC Wimbledon | 2.43 | 3.24 | 2.89 |
| 12. 20/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Stockport | 2.25 | 3.49 | 2.99 |
| 13. 20/08/22 | 17:00 | Dundee Utd vs St. Mirren | 2.31 | 3.09 | 3.24 |
| 14. 20/08/22 | 17:00 | Motherwell vs Livingston | 2.25 | 3.13 | 3.33 |
| 15. 20/08/22 | 17:00 | Ross County vs Kilmarnock | 2.26 | 3.14 | 3.29 |
| 16. 20/08/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Aberdeen | 2.93 | 2.98 | 2.58 |
| 17. 20/08/22 | 17:00 | Hamilton vs Raith Rovers | 2.43 | 3.14 | 2.99 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 17 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1527 | Cheongju FC vs Cheonan City FC | 2.75 | 2.90 | 2.55 |
| 13:00 | 2355 | JEF United Chiba vs Ventforet Kofu | 2.54 | 2.83 | 2.83 |
| 13:00 | 2934 | Gwangju vs Jeonnam Dragons | 1.70 | 3.54 | 4.33 |
| 13:00 | 4061 | Benfica Lisbon B vs CF Estrela | 1.76 | 3.59 | 4.18 |
| 13:00 | 5636 | Gyeongnam vs Daejeon Citizen | 2.75 | 3.43 | 2.25 |
| 13:30 | 1914 | Chungnam Asan vs Gimpo Citizen | 1.80 | 3.39 | 4.03 |
| 14:30 | 1286 | Wuhan Zall vs Beijing Guoan | 3.48 | 3.33 | 1.95 |
| 14:30 | 1772 | Henan Jianye vs Wuhan Three Towns FC | 5.30 | 4.22 | 1.48 |
| 14:30 | 5854 | Meizhou Kejia vs Guangzhou RF | 1.23 | 5.49 | 9.81 |
| 15:15 | 5151 | Sarawak vs FC Petaling Jaya City | 2.51 | 3.40 | 2.45 |
| 16:00 | 2935 | Kedah vs Sabah | 1.98 | 3.38 | 3.34 |
| 16:00 | 3454 | Selangor FC vs Terengganu | 1.81 | 3.53 | 3.77 |
| 16:00 | 4164 | Dodoma FC vs Mbeya City | 2.18 | 2.75 | 3.59 |
| 16:00 | 5045 | Coastal Union vs KMC | 2.29 | 2.80 | 3.55 |
| 17:00 | 1492 | Cruz Azul U20 vs Tijuana U20 | 1.92 | 3.34 | 3.59 |
| 17:00 | 2549 | Pakhtakor vs FC Olimpik | 1.16 | 5.71 | 15.74 |
| 17:25 | 2755 | Al Sadd SC vs Al Ahli Doha SC | 1.35 | 5.10 | 6.08 |
| 18:00 | 1079 | Nasaf Qarshi vs Otmk Olmaliq | 1.72 | 3.43 | 4.42 |
| 18:00 | 2849 | KS Sleza Wroclaw vs MKS Kluczbork | 1.47 | 4.42 | 5.11 |
| 18:00 | 3678 | Wieczysta Krakow vs Sokol Sieniawa | 1.13 | 8.20 | 14.00 |
| 18:00 | 4289 | Miedz II vs Rekord Bielsko Biala | 4.30 | 4.30 | 1.62 |
| 18:00 | 4907 | Concordia Elblag vs Legionovia | 5.00 | 4.10 | 1.57 |
| 18:15 | 3860 | Simba vs Geita Gold FC | 1.38 | 4.12 | 7.45 |
| 18:30 | 1182 | Nyiregyhaza vs Soroksar | 2.36 | 3.14 | 2.79 |
| 18:30 | 4560 | Dorogi FC vs Szentlorinc SE | 2.36 | 3.14 | 2.79 |
| 18:30 | 4591 | FK Sloga Simin Han vs NK Posusje | 2.05 | 3.20 | 3.60 |
| 19:00 | 1512 | Kapa vs Keski Uusimaa | 1.49 | 4.71 | 4.61 |
| 19:00 | 1564 | Hillerod vs FC Fredericia | 4.51 | 4.02 | 1.59 |
| 19:30 | 1936 | Vejgaard B vs FC Djursland | 1.39 | 5.00 | 6.20 |
| 19:30 | 2390 | ASA Aarhus vs Arhus Fremad 2 | 7.40 | 5.40 | 1.32 |
| 19:30 | 4802 | Kjellerup IF vs Odder Igf | 4.61 | 4.42 | 1.52 |
| 19:30 | 5571 | Enppi Club vs Talaea El Gaish | 2.71 | 2.81 | 2.86 |
| 19:35 | 1855 | Al-Shamal vs Al Gharafa SC | 3.68 | 3.73 | 1.79 |
| 19:45 | 2538 | Djurgardens IF vs Apoel Nicosia | 1.83 | 3.47 | 4.23 |
| 19:45 | 4518 | Karabakh vs Viktoria Plzen | 2.24 | 3.11 | 3.21 |
| 20:00 | 1699 | Vejle BK vs Naestved BK | 1.49 | 4.13 | 5.31 |
| 20:00 | 3013 | Budafoki Mte vs Gyirmot FC | 3.00 | 3.44 | 2.10 |
| 20:30 | 1632 | Bloemfontein Celtic vs Orlando Pirates | 3.35 | 2.85 | 2.32 |
| 21:00 | 2230 | Reynir Sandgerdi vs IR Reykjavik | 3.10 | 4.20 | 1.92 |
| 21:00 | 3390 | Volsungur vs Aegir | 2.17 | 3.93 | 2.60 |
| 21:45 | 1051 | Stoke City vs Middlesbrough | 2.57 | 3.17 | 2.67 |
| 21:45 | 2622 | Solihull Moors vs York City | 1.60 | 3.98 | 4.78 |
| 22:00 | 1905 | Dynamo Kiev vs Benfica | 4.61 | 3.71 | 1.68 |
| 22:00 | 3023 | Maccabi Haifa vs Red Star Belgrade | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 22:00 | 4160 | West Bromwich vs Cardiff | 1.62 | 3.69 | 5.18 |
| 22:00 | 4277 | Sheffield Utd vs Sunderland | 1.75 | 3.50 | 4.50 |
| 22:00 | 5183 | Reading vs Blackburn | 2.99 | 3.24 | 2.29 |
| 22:15 | 1092 | Haukar vs Njarovik | 3.85 | 4.40 | 1.68 |
| 22:30 | 3055 | CA Tigre vs Atletico Tucuman | 2.09 | 3.05 | 3.39 |
| 22:30 | 3872 | NewellS Old Boys vs Lanus | 1.85 | 3.23 | 4.01 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA, GEITA GOLD WATAFUTANA, MAKOCHA WAZIPANIA POINTI TATU

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiikaribisha Geita Gold FC leo katika mechi yao ya kwanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu 2022/23, makocha wa timu hizo, Zoran Maki na Mathias Wandiba, kwa nyakati tofauti kila mmoja amesema "hatuwadharau".

**Simba wataikaribisha Geita Gold FC katika mchezo huo utakaopigwa saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ukiwa ni wakukamilisha michezo ya raundi ya kwanza ya ligi hiyo iliyoanza rasmi Jumatatu wiki hii.**

Simba ikinolewa na Kocha Mserbia, Zoran, anajivunia kuwa na kikosi imara kulingana na ubora wa wachezaji aliokuwa nao kwa msimu huku Geita Gold FC nayo inayofundishwa na mzawa Fred Felix Minziro, nayo inajivunia kufanya maboresho makubwa katika kikosi chao msimu huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe jana, Zoran alisema hana majeruhi kuelekea mchezo wa kesho na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu katika mchezo huo dhidi ya Geita Gold FC.

Alisema baada ya kupoteza mchezo wao wa Ngao ya Jamii, amefanyia kazi mapungufu yao na wako tayari kwa mechi hiyo ya leo kwa kuwa wamejiandaa kisaikolojia na kiufundi kutafuta



matokeo mazuri.

"Maandalizi yetu yako vizuri na wachezaji wangu wapo tayari kutafuta matokeo mazuri ili kufikia malengo yetu ya kuanza kutafuta pointi tatu katika mchezo wetu wa kwanza kwa msimu mpya," alisema Zoran Maki.

Alisema watacheza kwa tahadhari kubwa kwa kuwaheshimu wapinzani wao kwa sababu ana imani nao wamejindaa kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo.

"Mechi itakuwa na ushindani mkubwa, lakini nimewaandaa wachezaji wangu kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri na ushindi mkubwa," alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Geita Gold FC, Wandiba alisema wameandaa kikosi chao kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi tatu dhidi ya Simba na kuhakikisha wanaendelea pale walipoishia msimu uliopita.

Alisema msimu uliopita walipata pointi dhidi ya wapinzani wao hao jambo ambalo wanahitaji kulifanya katika mchezo wao wa leo kwa kuondoka na pointi tatu.

"Simba ni timu kubwa wanauzoefu mkubwa kulingana na wachezaji waliokuwa nao, tunawaheshimu, hatuwaogopi, kesho (leo) tunahitaji kupata pointi tatu muhimu," alisema Wandiba.

# *Namungo, Mtibwa roho kwatu kwa sare*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya sare ya mabao 2-2 juzi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu za Namungo na Mtibwa Sugar zimeonyesha kuridhishwa na matokeo hayo.

Straika Reliants Lusajo ambaye msimu uliopita alianza na moto, lakini baadaye ukafifia na kuishia na mabao 10, alifunga mabao yote mawili kwenye mchezo huo, akisema lengo lake siyo kukimbizana na mbio za Kiatu cha dhahabu, bali kuisaidia timu yake.

Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma baada ya mechi hiyo juzi, alisema matokeo waliyoyapata ni bora kwao kwa sababu wanajihesabia walicheza wakiwa ugenini.

"Pamoja na kwamba hatukucheza Lindi, lakini tunajihesabia kuwa tuko ugenini kwa sababu hatupo nyumbani kwetu, kusema kweli hatukucheza vibaya na kwa matokeo tuliyoyapata ni bora. Katika soka makosa yapo na ndiyo maana tumefungwa mabao mawili makosa ambayo tutakwenda kurekebisha, lakini kizuri zaidi na sisi tumefunga mabao mawili tukiwa ugenini," alisema Awadh.



Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio', alisema mpira kwa sasa umebadilika sana nchini na timu yoyote inaweza kutoka sare, kushinda au kufungwa ikiwa nyumbani au ugenini.

"Unaweza kufungwa popote pale, Mtibwa Sugar nao wamejiandaa, inaonekana pia msimu huu ligi itakuwa ngumu kwa sababu ya uwezeshwaji kama tulivyokuwa tunacheza sisi miaka ya nyuma, timu nyingi zilipokuwa zikimilikiwa na mashirika ya umma, ligi ilikuwa ngumu. Kuna vitu tumevione kwenye mechi zinazokuja tutafanya vizuri," alisema Julio.

Michezo
Jumatano Agosti 17, 2022
Nipashe



Klopp akerwa kadi ya Nunez UKURASA 21

LA USHINDI...



Beki wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, akiifungia timu yake bao la ushindi wakati wakiichapa Polisi Tanzania mabao 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Dejan atoa ahadi ya mabao Simba

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kelele nyingi za mashabiki wa soka hususan wa Yanga kuwatania watani wao wa jadi, Simba kwamba 'wamepigwa' katika usajili wa straika Dejan Georgijevic kutokana na uwezo mdogo aliouonyesha kwenye michezo miwili, mshambuliaji huyo raia wa Serbia ameibuka na kusema "mabao yanakuja".

Katika michezo miwili Dejan aliyocheza, ule wa kirafiki dhidi ya Saint George ya Ethiopia na wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga Jumamosi, alitokea benchi zikiwa zimebaki si zaidi ya dakika 15, na hakuweza kuonyesha makali yake jambo ambalo mashabiki wa Yanga wamekuwa wakiendeleza utani wao kuwa Simba walipotea kwa kumsajili nyota huyo.

Hata hivyo, kuonyesha kwamba hajafurahishwa na ubora aliuonyesha katika mechi hizo, Dejan ameeleza kutofurahishwa na hali hiyo na kwamba anaumia sana kwa matokeo hayo.

"Licha ya ukweli kwamba nimekuwa sehemu ya familia ya Simba kwa siku chache, nashiriki maumivu, mfadhaiko kwa kupoteza mechi yetu dhidi ya wapinzani wetu wa jadi.

"Binafsi najihesabu niliyezaliwa kuwa mshindi kama raia mwenzangu, Novak Djokovic," alisema na kuongeza.

"Kwa heshima niliyo nayo kwa mamilioni ya mashabiki wa Simba nitapambana, nitajitahidi, nitajitolea na kufanya kila linalowezekana ili kutoa huduma bora kwa timu yangu kwa kufunga mabao na kuwafanya mashabiki kuwa na furaha, wajivunie na kuwa upande wa ushindi daima."

# Yanga yaanza ligi ilipoishia

## Mayele atetema lakini akosa penalti wakiipigisha kwata Polisi Tanzania, Mwamnyeto naye...

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ilivyokuwa kwenye Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara jana walitoka nyuma kwa bao moja na kufanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania, wakianza vema kutetea ubingwa wao.

**Straika wa timu hiyo, Fiston Mayele ameanza msimu kwa kufungua akaunti ya mabao, alipofunga bao moja, huku akiingia kwenye vitabu vya kumbukumbu ya kukosa mkwaju wa penalti.**

Beki wa Polisi Tanzania Mohamed Mmanga naye jana kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, alikuwa mchezaji wa kwanza msimu huu kulambwa kadi nyekundu, akiipata dakika ya 88 kwa kumchezea madhambi Heritier Makambo.

Yanga ingeweza kujipatia bao mapema tu sekunde ya 22, baada ya kipa wa Polisi Tanzania Kelvin Igenderezi kumpasia beki wake wa kulia, Hassan Kapona aliyekuwa amezubaa, mpira ukawahiwa na Gael Bigirimana na kupiga krosi fupi iliyozua kizaazaa langoni mwa timu hiyo, lakini bahati mabeki waliwahi kuokoa.

Mayele alikosa penalti dakika ya 11 iliyookolewa vema na Igenderezi, baada ya Juma Ramadhani kumsukuma Jesus Moloko ndani ya eneo la hatari.

Ilikuwa ni penalti ya pili kutolewa tangu mechi ya ufunguzi Jumatatu iliyopita, lakini zote zikikoswa.

Ibrahim Ally wa Namungo alikosa penalti kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, zikitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kona iliyochongwa na kiungo mshambuliaji mpya wa Yanga raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki dakika ya 17, ilimkuta Moloko aliyepiga kichwa cha kupunyua, mpira ukagonga mwamba wa juu kabla ya mabeki kuufagia.

Yanga iliendelea kukosa mabao kwani dakika nne baadaye, Mayele alikosa kuugusa tu mpira wa krosi ya Bigirimana ili uingie wavuni.

Hatimaye Polisi Tanzania walifanya shambulizi langoni mwa Yanga dakika ya 21, baada ya Idd Kipagwile kuwatoroka mabeki wa timu hiyo na kuachia kombora lililopaa juu ya lengo.

Maafande walifanikiwa kuandika bao dakika ya 33 lililofungwa na Salum Kipemba. Alikuwa ni yeye mwenyewe Kipemba aliyeondoka na mpira katikati ya uwanja, akampasia Salum Chuku kwenye wingi ya kushoto ambaye alipiga krosi iliyomkuta beki Bakari Mwamnyeto katika harakati ya kuuokoa mpira huo ukampiga Kipemba mguuni na kurudi golini kwa Yanga ukajaa wavuni kipa Djigui Diarra akiwa amepotea maboya.

Yanga ilisawazisha bao hilo dakika nane baadaye kupitia kwa Mayele ambao aliukuta mpira uliokuwa umeokolewa kizembe na mabeki wa Polisi Tanzania, akaukwamisha wavuni.

Kipindi cha pili baada ya mabadiliko ya pande zote mbili, Yanga ilionekana kuutawala mpira zaidi kuliko wapinzani wao.

Ni kipindi ambacho ilifanya shambulizi moja pekee la hatari dakika ya 57 lililotokana na mkwaju wa faulo iliyopigwa na Rajab Athumani, lakini uhodari wa Diarra uliiokoa Yanga.

Kuanzia dakika ya 70, Mabingwa Watetezi walihamia kwenye lango la maafande hao, ambao walionekana wamechoka na kufanya makosa mengi na ilionekana kabisa kuwa wangeruhusu bao.

Dakika tano kabla mpira haujamalizika, baada ya sekeseke nyingi, hatimaye beki Bakari Mwamnyeto alipeleka ushindi Jangwani kwa kupachika bao la pili, akimalizia mpira wa kona iliyopigwa na Bernard Morrison aliyeingia kipindi cha pili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >